

KITABU CHA 'NNE CHA MUSA

HESABU.



ZANZIBAR :

PRINTED AT THE UNIVERSITIES' MISSION PRESS.

1887.

KITABU CHA 'NNE CHA MUSA.

HESABU.

SURA 1.

A KASEMA Bwana kwa Musa katika bara ya Sinai, hemani mwa kusanyiko, siku ya kwanza ya mwezi wa pili, mwaka wa pili baada ya kutoka inchi ya Misri, 2 akisema, Fanyeni hesabu ya kusanyiko lote la waana wa Israeli, kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa hesabu ya majina, killa mume, kwa vitwa vyao: 3 wenyi miaka asharini na zayidi, wote wawezao kwenda vitani kwa Israeli, wewe na Harun mtawahesabu kwa majeshi yao. 4 Na pamoja nanyi patakuwa wa killa kabila mtu mmoja, killa mmoja juu ya nyumba ya 5 babaze. Na haya majina ya watu watakao-simama nawe: wa Reuben; Elizur mwana 6 wa Shedeur. Wa Simeon; Shelumiel 7 mwana wa Zurishaddai. Wa Yuda; Na-shon mwana wa Amminadab. Wa Issakar; 8 Nethanel mwana wa Zuar. Wa Zabulon; 9 Eliab mwana wa Helon. Wa waana wa Yusuf: wa Efraim; Elishama mwana wa Ammihud: wa Manasse; Gamaliel mwana wa 11 Pedazur. Wa Benjamin; Abidan mwana 12 wa Gideoni. Wa Dan; Ahiezer mwana wa

- 13 Ammishaddai. Wa Asher ; Pagiel mwana
 14 wa Okran. Wa Gad ; Eliasaf mwana wa
 15 Deuel. Wa Naftali ; Ahira mwana wa
 16 Enan. Hawa ndio waliokwitwa wa kusa-
 nyiko, wakuu wa makabila ya baba zao ; ha-
 17 wa walio juu yao elfu za Israeli. Musa na
 Harun wakawatwaa hawa waliotajwa maji-
 18 na : wakawakusanya kusanyiko lote ya kwa-
 nza ya mwezi wa pili, wakatangaza vizazi
 vyao kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba
 zao, kwa hesabu ya majina, wenyi miaka
 19 asharini na zayidi, kwa vitwa vyao. Bwana
 alivyomwamuru Musa, ndivyo alivyowa-
 hasibu katika bara ya Sinai.
- 20 Na waana wa Reuben, mzaliwa wa kwa-
 nza wa Israeli, vizazi vyao, kwa jamaa zao,
 kwa nyumba za baba zao, kwa hesabu ya
 majina, kwa vitwa vyao, killa mume mwe-
 nyi miaka asharini na zayidi, wote walio-
 21 weza kwenda vitani; waliohesabiwa wao,
 wa kabila la Reuben, elfu sita u arobaini, na
 mia tano.
- 22 Wa waana wa Simeon, vizazi vyao,
 kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao,
 wale waliohesabiwa wao, kwa hesabu ya
 majina, kwa vitwa vyao, killa mume mwe-
 nyi miaka asharini na zayidi, wote walio-
 23 weza kwenda vitani ; waliohesabiwa wao,
 wa kabila la Simeon, elfu tissia u hamsini na
 mia tatu.
- 24 Wa waana wa Gad, vizazi vyao, kwa ja-
 maa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa he-
 sabu ya majina, wenyi miaka asharini na

- zayidi, wote walioweza kwenda vitani ;
25 waliohesabiwa wao wa kabila la Gad, elfu
hamsi u arobaini mia sita na hamsini.
- 26 Wa waana wa Yuda, vizazi vyao, kwa
jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa
hesabu ya majina, wenyi miaka asharini
27 na zayidi, wote walioweza kwenda vitani ;
waliohesabiwa wao, wa kabila la Yuda, elfu
aroba u sabwini na mia sita.
- 28 Wa waana wa Issakar, vizazi vyao, kwa
jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa
hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na
zayidi, wote walioweza kwenda vitani ;
29 waliohesabiwa wao, wa kabila la Issakar,
elfu aroba u hamsini na mia 'nne.
- 30 Wa waana wa Zabulon, vizazi vyao, kwa
jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa
hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na
zayidi, wote walioweza kwenda vitani ;
31 waliohesabiwa wao, wa kabila la Zabulon,
elfu saba u hamsini na mia nne.
- 23 Wa waana wa Yusuf, waana wa Efraim,
vizazi vyao, kwa jamaa zao, kwa nyumba
za baba zao, kwa hesabu ya majina, wenyi
miaka asharini na zayidi, wote walioweza
33 kwenda vitani ; waliohesabiwa wao, wa ka-
bila la Efraim, elfu arobaini na mia tano.
- 34 Wa waana wa Manasse, vizazi vyao, kwa
jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa
hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na
35 zayidi, walioweza kwenda vitani ; waliohe-
sabiwa wao, wa kabila la Manasse, elfu
theneen u thelathini na mia mbili.

- 36 Wa waana wa Benjamin, vizazi vyao, kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na zayidi, wote walioweza kwenda vitani;
- 37 waliohesabiwa wao, wa kabila la Benjamin, elfu hamsi u thelathini na mia 'nne.
- 38 Wa waana wa Dan, vizazi vyao, kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na zayidi, wote walioweza kwenda vitani;
- 39 waliohesabiwa wao, wa kabila la Dan, elfu theneen u settini na mia saba.
- 40 Wa waana wa Asher, vizazi vyao, kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na zayidi, wote walioweza kwenda vitani;
- 41 waliohesabiwa wao, wa kabila la Asher, elfu wahid u arobaini na mia tano.
- 42 Wa waana wa Naftali, vizazi vyao, kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, kwa hesabu ya majina, wenyi miaka asharini na zayidi, wote walioweza kwenda vitani; waliohesabiwa wao, wa kabila la Naftali, elfu thelatha u hamsini na mia nne.
- 43
- 44 Hawa waliohesabiwa, waliowahasibu Musa na Harun, na wakuu wa Israeli, watu thenashara : akawa killa mmoja kwa nyumba ya baba zake. Bassi wote waliohesabiwa wa waana wa Israeli kwa nyumba za baba zao, wenyi miaka asharini na zayidi, wote walioweza kwenda vitani wa Israeli; hatta
- 45 wale wote waliohesabiwa walikuwa elfu sita
- 46 mia na tatu, na mia tano, na hamsini.

47 Lakini Walawi kwa kabila la baba zao
 48 hawakuhesabiwa kati mwao. Kwani Bwa-
 49 na alimwambia Musa, akisema, Kabila
 la Lawi tu usiwahasibu, wala usifanye he-
 50 sabu yao kati ya waana wa Israeli : lakini
 uwaagize Walawi juu ya masikani ya usha-
 hidi, na juu ya vyombo vyake vyote, na
 juu ya vitu vyake vyote: wataichu-
 kua masikani, na vyombo vyake vyote :
 nao wataingojea, na watatua wakiizungu-
 51 ka masikani. Nayo masikani itakapoende-
 lea, Walawi watakaoishusha : na masikani
 itakapotandikwa Walawi watakaoipandi-
 sha : na mgeni atakayeikaribia atauawa.
 52 Nao waana wa Israeli watatanda hema zao,
 killa mtu penyi matuo yake na killa mtu
 53 penyi bendera yake kwa majeshi yao. La-
 kini Walawi watatua pande za masikani ya
 ushahidi, isiwe ghathabu juu ya kusanyiko
 la waana wa Israeli : nao Walawi watalinda
 54 malinzi ya masikani ya ushahidi. Ndivyo
 walivyofanya waana wa Israeli : kwa yote
 Bwana aliyomwamuru Musa, ndivyo wali-
 vyofanya.

SURA 2.

2 **B**WANA akawaambia Musa na Harun,
 akisema, Waana wa Israeli watatua
 killa mtu penyi bendera yake kwa
 ishara za nyumba za baba zao : kuelekea
 hema ya kusanyiko watatua pande zote.
 3 Nao watuao upande wa mashariki, kwa

jeshi yao. Nao wa pili watakaotoka.

- 17 Ndipo hema ya kusanyiko itatoka, na matuo ya Walawi katikati ya matuo : kama watuavyo ndivyo watakavyoendelea, killa mtu na mahali pake, kwa bendera zao.
- 18 Upande wa magharibi bendera ya matuo ya Efraim kwa majeshi yao : na mkuu wa waana wa Efraim Elishama mwana wa
- 19 Ammihud. Na jeshi lake, nao waliohesabi-
- 20 wa kwao, elfu arobaini na mia tano. Na karibu yake kabila la Manasse : na mkuu wa waana wa Manasse Gamaliel mwana wa Pe-
- 21 dazur : na jeshi lake, nao waliohesabiwa kwao, elfu theneen u thelathini na miteen :
- 22 na kabila la Benjamin : na mkuu wa waana wa Benjamin Abidan mwana wa Gideo-
- 23 ni : na jeshi lake, nao waliohesabiwa kwao,
- 24 elfu hamsi u thelathini, na mia 'nne. Wote waliohesabiwa wa matuo ya Efraim elfu mia na nane, na mia, kwa majeshi yao. Nao wa tatu watakaotoka.
- 25 Upande wa kaskazini bendera ya matuo ya Dan kwa majeshi yao : na mkuu wa waana wa Dan Ahiezer mwana wa Ammi-
- 26 shaddai. Na jeshi lake, nao wote waliohesabiwa kwao, elfu theneen u settini na mia
- 27 saba. Nao watuao karibu yake kabila la Asher : na mkuu wa waana wa Asher
- 28 Pagi el mwana wa Okran : na jeshi lake, nao waliohesabiwa kwao, elfu wahid u arobaini na mia tano : na kabila la Naftali ;
- 29 na mkuu wa waana wa Naftali Ahira
- 30 mwana wa Enan : na jeshi lake, nao

- waliohesabiwa kwao, elfu thelatha u hamsi-
 31 ni na mia 'nne. Wote waliohesabiwa wa ma-
 tuo ya Dan elfu mia na hamsini na saba,
 na mia sita. Nao watatoka wa mwisho kwa
 bendera zao.
- 32 Hawa waliohesabiwa wa waana wa Isra-
 eli kwa nyumba za baba zao : wote walio-
 hesabiwa wa matuo kwa majeshi yao elfu
 sita mia na tatu na mia tano na hamsini.
- 33 Lakini Walawi hawakuhesabiwa katika
 waana wa Israeli ; kama Bwana alivyo-
- 34 mwamuru Musa. Ndivyo walivyofanya
 waana wa Israeli ; kwa yote Bwana aliyo-
 mwamuru Musa, ndivyo walivyotua kwa
 bendera zao, ndivyo walivyotoka, killa
 mmoja kwa jamaa zao, kwa nyumba za
 baba zao.

SURA 3.

- B**ASSI hivi vizazi vya Harun na Musa
 siku aliposema Bwana na Musa kati-
 2 ka mlima Sinai. Na haya majina ya waana
 wa Harun ; Nadab mzaliwa wa kwanza, na
 3 Abihu, Eleazar, na Ithamar. Haya majina
 ya waana wa Harun, wakohani waliotiwa
 mafuta, aliowajaza mikono wangojee kazi
 4 ya kikohani. Wakafa Nadab na Abihu
 mbele ya Bwana walipotoa moto mgeni
 mbele ya Bwana, katika bara ya Sinai,
 wala kwao hapana watoto ; wakaingojea
 kazi ya kikohani Eleazar na Ithamar ma-
 choni pa Harun baba yao.
- 5 Bwana akamwambia Musa, akisema,

- 6 Uwakaribishe kabila la Lawi, ukawaweke
7 mbele ya Harun mkohani, wamngojee. Nao
watayalinda malinzi yake, na malinzi ya
kusanyiko lote mbele ya hema ya kusanyi-
8 ko, kuhudumia huduma ya masikani. Nao
watavitunza vyombo vyote vya hema ya
kusanyiko, watalinda malinzi ya waana wa
Israeli, kuhudumia huduma ya masikani.
- 9 Nao Walawi utampa Harun na waanawe ;
kupewa amepewa hawa kwa ajili ya waana
10 wa Israeli. Nawe utamwagiza Harun, na
waanawe, nao wataushika ukohani wao :
na mgeni atakayekaribia, atauawa.
- 11 Bwana akamwambia Musa, akisema, Na-
12 mi, angalia, nimewatwaa Walawi katika
kati ya waana wa Israeli mahali pao waume
wa kwanza wafunguao tumbo la mama kati
ya waana wa Israeli : nao Walawi wataku-
13 wa wangu ; kwani waume wa kwanza wote
wangu ; siku nilipowapiga waume wa kwa-
nza wote katika inchi ya Misri ndipo nili-
pojitakasia waume wa kwanza wote wa
Israeli, wa watu na wa nyama : wangu wa-
takuwa : ndimi Bwana.
- 14 Bwana akamwambia Musa katika bara
15 ya Sinai, akisema, Uwahasibu waana wa
Lawi kwa nyumba za baba zao, kwa jamaa
zao ; killa mume mwenyi mwezi na zayidi
16 utawahasibu. Musa akawahasibu kwa
neni la Bwana, kama alivyoamuriwa.
- 17 Wakawa hawa waana wa Walawi kwa ma-
jina yao ; Gershon, na Kohath, na Merari.
18 Na haya majina ya waana wa Gershon

- 19 kwa jamaa zao; Libni na Shimei. Na waana wa Kohath kwa jamaa zao; Amram, 20 na Izhar, Hebron, na Uzziel. Na waana wa Merari kwa jamaa zao; Mahli na Mushi. Hizi jamaa za Walawi kwa nyumba za baba zao.
- 21 Wa Geshon jamaa ya Walibni, na jamaa ya Washimei: hawa jamaa za Wagershoni. 22 Waliohesabiwa wao, kwa hesabu ya waume wote, waliopata mwezi na zayidi, walio- 23 hesabiwa wao, elfu saba na mia tano. Jamaa za Wagershoni watatua nyuma ya 24 masikani kwa magharibi. Na mkuu wa nyumba ya baba za Wagershoni Eliasaf 25 mwana wa Lael. Na kutunza kwa waana wa Gershon katika hema ya kusanyiko watatunza masikani na ile hema, funiko lake, na tandiko la mlango wa hema ya 26 kusanyiko, na machandalua ya ua, na tandiko la mlango wa ua, ulioko kwa masikani, na kwa mathbahu pande zake, na kamba zake za huduma yake yote.
- 27 Na wa Kohathi jamaa ya Waamram, na jamaa ya Waizhar, na jamaa ya Wahebron, na jamaa ya Wauzziel: hawa jamaa za 28 Wakohathi. Kwa hesabu ya waume wote, waliopata mwezi na zayidi, elfu nane na sita mia, wakilinda malinzi ya patakatifu. 29 Jamaa za waana wa Kohath watatua upa- 30 nde wa masikani wa kusini. Na mkuu wa nyumba ya baba za jamaa za Wakohath 31 Elizafan mwana wa Uzziel. Na kutunza kwao watatunza sanduku, na meza, na ki-

nara, nazo mathbahu, na vyombo vya patakatifu, wangojeleavyo, na tandiko na
 32 huduma yake yote. Na Eleazar, mwana wa Harun mkohani, mkuu wa wakuu wa Walawi, awasimamie walindao malinzi ya patakatifu:

33 Wa Merari jamaa ya Wamahli, na jamaa
 34 ya Wamushi: hizi jamaa za Merari. Nao waliohesabiwa wao, kwa hesabu ya waume wote, waliopata mwezi na zayidi, elfu sita
 35 na miteen. Na mkuu wa nyumba ya baba za jamaa za Merari Zuriel mwana wa Abihail: watatua upande wa masikani wa
 36 kaskazini. Na usimamizi wao waana wa Merari kutunza mbau za masikani, na michukuzi yake, na nguzo zake, na maweko yake, na vyombo vyake vyote, na
 37 huduma yake yote; na nguzo za ua pande zote, na maweko yao, na mismari yao, na
 38 kamba zao. Nao watuao mbele ya masikani kwa mashariki, mbele ya hema ya kusanyiko kwa kutokea jua, Musa, na Harun na waanawe, wakilinda malinzi ya patakatifu kwa malinzi ya waana wa Israeli; naye mgeni atakayekaribia, atauawa.
 39 Wote waliohesabiwa wa Walawi, Musa na Harun waliowahasibu kwa amri ya Bwana, kwa jamaa zao, waume wote waliopata mwezi na zayidi, elfu theneen asharini.
 40 Bwana akamwambia Musa, Uwasibusu waume wote wazaliwa wa kwanza wa waana wa Israeli, waliopata mwezi na zayidi,
 41 ukafanye hesabu ya majina yao. Nawe uta-

- nitwalia Walawi, (ndimi Bwana) mahali pao wazaliwa wa kwanza wote wa kati ya waana wa Israeli; na makundi ya Walawi mahali pao wazaliwa wa kwanza wa kati ya makundi yote ya waana wa Israeli. Musa akawahasibu, kama Bwana alivyomwamuru, wazaliwa wa kwanza wote kati ya waana wa Israeli. Na waume wote wazaliwa wa kwanza kwa hesabu ya majina, waliopata mwezi na zayidi, katika wale waliohesabiwa wao, elfu theneen u asharini, na miteen, na thelatha u sabwini.
- 44 Bwana akamwambia Musa, akisema,
 45 Uwatwae Walawi mahali pa wazaliwa wa kwanza wote kati ya waana wa Israeli, na makundi ya Walawi mahali pa makundi yao: na Walawi watakuwa wangu; ndimi
 46 Bwana. Na kwa kuwakomboa wale miteen na thelatha u sabwini wazaliwa wa kwanza wa waana wa Israeli, waliowasazia Walawi,
 47 utawatwalia shekeli tano tano killa mmoja; kwa shekeli ya patakatifu utatwaa (shekeli ni gera asharini): nawe utawapa Harun na waanawe fetha, watakayokombolelea
 49 hesabu yao iliyosazwa. Musa akawatwalia fetha ya ukombozi waliowasazia wao
 50 waliokombolewa na Walawi: waliozaliwa wa kwanza wa waana wa Israeli ndio alio watwalia fetha, elfu na mia tatu, na settini na tano, kwa shekeli ya patakatifu:
 51 Musa akawapa Harun na waanawe fetha ya ukombozi, kwa neno la Bwana, kama Bwana alivyomwamuru Musa.

SURA 4.

BWANA akamwambia Musa na Harun,
 2 akisema, Fanyeni hesabu ya waana
 wa Kohath katika kati ya waana wa Lawi,
 kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao,
 3 waliopata miaka thelathini na zayidi hatta
 miaka hamsini, wote waingiao serikari,
 kuifanya kazi katika hema ya kusanyiko.
 4 Hii huduma ya waana wa Kohath katika
 hema ya kusanyiko, matakatifu ya mata-
 5 katifu: matuo yatakapoendelea, Harun ata-
 ingia, na waanawe, nao wataishusha pazia
 ya tandiko, na kulifunikiza nayo sanduku la
 6 ushahidi: na wataweka juu yake funiko
 la ngozi za tahashi, na kutandaza juu
 nguo ya samawati yote, na kuingiza mi-
 7 chukuzi yake. Na juu ya meza ya mika-
 te ya wonyesho watatandaza nguo ya sa-
 mawati, na wataweka juu yake sahani, na
 miiko, na mabakuli na vikombe vya kumi-
 minia na mkate wa dayima utakuwa juu
 8 yake: nao watatandaza juu yao nguo ya
 nyekundu, na hiyo wataifunika na funiko
 la ngozi za tahashi, na kuingiza michukuzi
 9 yake. Nao watatwaa nguo ya sama-
 wati, na kufunikiza kinara cha nuru, na
 taa zake, na makoleo yake, na viweko vya-
 ke, na vyombo vyake vyote vya mafuta,
 10 wavingojeleavyo kwake: na kukitia, na
 vyombo vyake vyote ndani ya funiko la
 ngozi za tahashi, na kukiweka juu ya
 11 mti. Na juu ya mathbahu ya thahabu

- watatandaza nguo ya samawati, na kuifunikiza na funiko la ngozi za tahashi, na
- 12 kuingiza michukuzi yake : nao watavitwaa vyombo vyote vya ungoje, wavingojelevyo katika patakatifu, na kuvitia katika nguo samawati, na kuvifunikiza na funiko la ngozi za tahashi, na kuviweka katika
- 13 mti. Nao watayaondoa majifu mathbahuni, na kutandaza nguo ya urujuani juu
- 14 yake : nao wataweka juu yake vyombo vyake vyote, waingojelevyo, vyetezo, mauma, na magembe, na mabakuli, vyombo vyote vya mathbahu ; nao watatandaza juu yake funiko la ngozi za tahashi, na kuingiza michukuzi yake. Na Harun na
- 15 waanawe watakapokwisha kufunikiza patakatifu, na vyombo vyote vya patakatifu, yakiwa matuo yataendelea ; baadaye, waana wa Kohath watakuja kuchukua : lakini patakatifu hawatagusa, wasife. Vitu hivi mzungo wa waana wa Kohath katika hema ya
- 16 kusanyiko. Na usimamizi wake Eleazar mwana wa Harun mkohani mafuta ya taa, na vukizo la manukato, na sadaka ya unga ya dayima, na mafuta ya kutika usimamizi wa masikani yote na wa yote yaliyomo, patakatifu na vyombo vyake.
- 17 Bwana akawaambia Musa na Harun
- 18 akisema, Msiwakatie mbali kabila la jamaa za Wakohath katika Walawi: haya
- 19 mwafanyie, wapate kuishi, wasife, wayakaribiapo matakatifu ya matakatifu : Harun na waanawe wataingia, na kuwaagi-

zia killa mtu huduma yake na mzigo wa-
20 ke: wala hawataingia kutazama hatta ki-
dogo patakatifu, wasife.

21 Bwana akamwambia Musa, akisema,
22 Fanya hesabu ya waana wa Gershon nao,
kwa nyumba za baba zao, kwa jamaa zao ;
23 waliopata miaka thelathini na zayidi hatta
miaka hamsini utawahasibu; wote wai-
ngiao kungojea serikari, kuhudumia hudu-
24 ma katika hema ya kusanyiko. Hii huduma
yao jamaa za Wagershoni, kwa kuhudumia
25 na kwa kuchukua mizigo: watachukua
mapazia ya masikani, na hema ya kusanyi-
ko, funiko lake, na funiko la ngozi za ta-
hashi lilioko juu yake, na tandiko la mla-
26 ngo wa hema ya kusanyiko; na machanda-
lua ya ua, na tandiko la mlango, mlango ni pa
ua, ulioko kwa masikani na kwa mathbahu
pande zake, na kamba zao, na vyombo
vyote vya huduma yao, nayo yote yata-
kayofanyika kwao, ndiyo watakayohudu-
27 mia. Kwa amri ya Harun na waanawe
itakuwa huduma yote ya waana wa Wa-
gershoni, kwa mizigo yao yote, na kwa
huduma yao yote: nanyi mtawasimamia
28 mizigo yao yote katika malinzi yao. Hii
huduma ya jamaa za waana wa Wagershoni
katika hema ya kusanyiko: na malinzi yao
chini ya mkono wa Ithamar mwana wa
Harun mkohani.

29 Waana wa Merari utawahasibu kwa ja-
30 maa zao, kwa nyumba za baba zao; walio-
pata miaka thelathini na zayidi hatta kwa

- miaka hamsini utawahasibu, killa mmoja aingiaye serikari, kuihudumia huduma ya
- 31 hema ya kusanyiko. Na haya malinzi ya mizigo yao, kwa huduma yao yote katika hema ya kusanyiko; mbau za masikani, na michukuzi yake, na nguzo zake, na
- 32 maweko yake; na nguzo za ua pande zote, na maweko yao, na mismari yao, na kamba zao, pamoja na vyombo vyao vyote, na huduma yao yote: na kwa jina mtawaagiz
- 33 zia vyombo vya malinzi ya mizigo yao. Hii huduma ya jamaa za waana wa Merari, kwa huduma yao yote, katika hema ya kusanyiko, chini ya mkono wa Ithamar mwana wa Harun mkohani.
- 34 Na Musa na Harun na wakuu wa kusanyiko wakawahasibu waana wa Wakohath kwa jamaa zao, na kwa nyumba za baba
- 35 zao, waliopata miaka thelathini na zayidi hatta kwa miaka hamsini, killa mmoja aingiaye serikari kwa huduma ya hemani mwa
- 36 kusanyiko; wakawa waliohesabiwa wao kwa jamaa zao elfeen na mia saba na hamsini.
- 37 Hawa waliohesabiwa wa jamaa za Wakohath, wote waliohudumia katika hema ya kusanyiko, Musa na Harun waliowahasibu kwa amri ya Bwana kwa mkono wa Musa.
- 38 Nao waliohesabiwa wa waana wa Gershon, kwa jamaa zao, na kwa nyumba za
- 39 baba zao, waliopata miaka thelathini na zayidi hatta kwa miaka hamsini, killa mmoja aingiaye serikari, kwa huduma

- 40 katika hema ya kusanyiko, hatta wale waliohesabiwa wao, kwa jamaa zao, kwa nyumba za baba zao, wakawa elfeen na
- 41 mia sita na thelathini. Hawa ndio waliohesabiwa wa jamaa za waana wa Gershon, wote waliohudumia katika hema ya kusanyiko, Musa na Harun waliowahasibu kwa amri ya Bwana. .
- 42 Nao waliohesabiwa wa jamaa za waana wa Merari kwa jamaa zao, kwa nyumba za
- 43 baba zao, waliopata miaka thelathini na zayidi hatta kwa miaka hamsini, killa mmoja aingiaye serikari kwa huduma
- 44 katika hema ya kusanyiko, hatta wale waliohesabiwa wao, kwa jamaa zao, wakawa
- 45 elfu tatu na miteen. Hawa ndio waliohesabiwa wa jamaa za waana wa Merari, Musa na Harun waliowahasibu kwa amri ya Bwana kwa mkono wa Musa.
- 46 Wale wote waliohesabiwa wa Walawi, waliowahasibu Musa na Harun na wakuu wa Israeli, kwa jamaa zao, na kwa nyumba za
- 47 baba zao, waliopata miaka thelathini na zayidi hatta kwa miaka hamsini, killa mmoja aingiaye kuhudumia huduma, na huduma ya mizigo, katika hema ya kusanyiko, hatta wale waliohesabiwa wao, wakawa elfu nane na mia tano na themanini.
- 48 Kwa amri ya Bwana waliohesabiwa kwa mkono wa Musa, killa mmoja kwa huduma yake, na kwa mzungu wake: ndivyo waliohesabiwa naye, kama Bwana alivyomwamuru Musa.

SURA 5.

- B**WANA akamwambia Musa, akisema,
 Uwaamuru waana wa Israeli, watoe
 matuoni killa mwenyi ukoma, na killa
 2 mwenyi kisunono, naye yote aliyejinajisi
 3 kwa mfu. Mume kwa mke mtawatoa, nje
 ya matuo mtawatoa, wasiyanajisi matuo
 4 yao, nikaaye kati mwake. Waana wa
 Israeli wakafanya hivi, huwatoa nje ya
 matuo : kama Bwana alivyomwambia Musa,
 kwa hivi hufanya waana wa Israeli.
- 5 Bwana akamwambia Musa, akisema,
 6 Uwaambie waana wa Israeli, mtu ataka-
 pofanya thambi mume ao mke, kama hufa-
 nyavyo waana Adamu, kumwasi Bwana,
 7 roho ile kuwa na hatiya ; ndipo wataungama
 thambi yao waliyoifanya ; naye atatoa mali-
 po ya kosa lake kamili, na kuyaongeza se-
 hemu ya tano, na kumpa yule aliyemkosa.
- 8 Lakini kama mtu hana jamaa wawezao ku-
 lipwa kosa, malipo ya kosa aliyofanyiziwa
 Bwana, yatakuwa ya mkohani ; pamoja na
 kondoo mume wa upatanisho, atakayepa-
 9 tanishwa naye. Na killa cha kuinua cha
 matakatifu yote ya waana wa Israeli, wata-
 kachomtolea mkohani, kitakuwa chake.
- 10 Na ya killa mtu yaliyotakasika yatakuwa
 yake : cho chote mtu atakachompa mkohani
 kitakuwa chake.
- 11 Bwana akamwambia Musa, akisema,
 12 Unene nao waana wa Israeli, ukawaambie,

- Kama mke wa mtu atembea, kama amfa-
 13 nyia kosa, na mwana mume alala naye kwa
 asharati, na kufichwa machoni pa mumewe,
 na kusettiri, naye amejinajisi, wala hapana
 shahidi juu yake, wala hakushikwa ;
 14 na yule *mume* akiingiliwa uwivu moyoni,
 akimwonea uwivu mke wake, naye kuwa
 na unajisi : ao akiingiliwa uwivu moyoni,
 akimwonea uwivu mke wake, naye hana
 15 unajisi : bassi mume atamletea mkohani
 mkewe, na matoleo yake atayachukua naye,
 sehemu ya kumi ya efa ya shayiri ; asimi-
 mine mafuta juu yake, wala asitie lebona :
 kwani sadaka ya unga ya uwivu hii, sada-
 ka ya unga ya ukumbusho, ikumbushayo
 16 uovu. Naye mkohani atamkaribisha, ata-
 17 mweka mbele ya Bwana ; na mkohani ata-
 twaa maji matakatifu chomboni mwa udo-
 ngo ; na mavumbi yaliyoko chini katika
 masikani atatwaa mkohani atayatia majini :
 18 naye mkohani atamweka mwanamke mbele
 ya Bwana, atamfunulia kitwa mwanamke,
 na sadaka ya unga ya ukumbusho atamwe-
 kea mikononi, iliyo sadaka ya unga ya
 uwivu : na mkohani atakuwa nayo mkono-
 19 ni maji ya uchungu ya kulaanisha : na mko-
 hani atamwapiza na kumwambia mwanam-
 ke, Asipokuwa mwanamume amelala
 nawe, nawe usipokuwa umetembea kwa
 asharati katika mume wako, uachiliwe na
 20 maji haya ya uchungu yalaanishayo : la-
 kini kama umetembea katika mume wako,
 nawe umetiwa unajisi, na mtu amelala na-

- 21 we zayidi ya mume wako : ndipo mkohani
 atamwapiza mwanamke kwa laana, na
 mkohani atamwambia mwanamke, Bwana
 akufanye laana na kiapo kati ya watu wa-
 ko, Bwana atakapokuangamizia paja, na ku-
 22 kuvimbishia tumbo ; na maji haya yalaani-
 shayo yataingia ndani mwako, na kuku-
 vimbishia tumbo, na kukuangamizia paja :
 na mwanamke atasema, Amin, Amin.
- 23 Na mkohani atayaandika malaana haya ki-
 tabuni, naye atayazimiliza kwa maji ya u-
 24 chungu: na atamnyweshwa yule mwanamke
 maji ya uchungu yalaanishayo: na maji
 yalaanishayo yatamwingia, machungu.
- 25 Na mkohani atatwaa ile sadaka ya unga ya
 uwivu mkononi kwa mwanamke, ataitikisa
- 26 mbele ya Bwana, ataileta kwa mathbahu :
 na mkohani atatwaa ukufi wa sadaka ya
 unga kwa ukumbusho wake, na kuchoma
 mathbahuni, halafu atamnyweshwa mwana-
 27 mke maji. Na akiisha kumnyweshwa maji,
 itakuwa kama ametiwa unajisi, na kumkosa
 mumewe, yale maji yalaanishayo yatamwi-
 ngia machungu, na tumbo lake litavimba, na
 paja lake litaangamia : naye mwanamke
 28 atakuwa laana kati ya watu wake. Hatta
 mwanamke asipotiwa unajisi, lakini yu
 safi ; ndipo ataachiliwa, atachukua mi-
 29 mba. Hii sheria ya uwivu, mke ataka-
 potembea katika mume wake, na kutiwa
 30 unajisi ; ao uwivu ukimwingilia mtu moyo-
 ni, naye amwonea uwivu mkewe, bassi ata-
 mweka mwanamke mbele ya Bwana, na

31 mkohani atamfanyizia sheria hii yote. Naye mwanamume ataachiliwa uovu, na yule mwanamke atauchukua uovu wake.

SURA 6.

BWANA akamwambia Musa, akisema, (2) Useme na waana wa Israeli, ukawa-ambie, Atakapojitenga mtu mume ao mke kwa kuweka nathiri ya Mnathiri, ajifanye
 3 wakf kwa Bwana: atakuwa wakf katika mvinyo na kileo; hatakunywa siki ya mvinyo, wala siki ya kileo, wala hatakunywa maji yo yote yatokayo zabibu, wala kula zabibu ao mbichi ao zilizokauka. Siku zote za nathiri yake hatakula kilichofanyika kwa mzabibu wa mvinyo, tangu makokwa hatta
 4 maganda. Siku zote za nathiri yake ya kuwa wakf hautamjia wembe kitwani; hatta siku zake za kujifanya wakf kwa Bwana zita-
 5 takapotimia, atakuwa mtakatifu, ataacha nyele za kitwani zikue. Siku zote za kujifanya wakf kwa Bwana hatakaribia mayiti.
 6 Asijitie uchafu kwa baba, ao kwa mama, kwa ndugu, ao kwa umbu, wakifa: kwa saba-
 7 babu kitwani kwake kuwa wakf kwa Muungu. Siku zote za kuwa wakf yu mtakatifu
 8 kwa Bwana. Na akifa mfu kwa ghafula karibu naye, na kitwa chake cha kuwa wakf kiki-
 9 tiwa uchafu, bassi atanyoa kitwa siku ya kutakasika kwake, siku ya saba atanyoa.
 10 Na siku ya nane atamletca mkohani mlangoni mwa hema ya kusanyiko hua wawili,

- 11 ao makinda ya njiwa wawili : na mkohani atamtoa mmoja wa thambi, na wa pili kwa kafara, atamfanyia upatanisho, akiwa amekosa kwa mayiti, na kitwa chake atatakasa siku ile ile. Naye atazifanya wakf kwa Bwana siku zake za kuwa wakf, naye ataleta mwana kondoo mume wa mwaka wa kwanza matoleo ya kosa : lakini siku za kwanza zitafunguka, kwa kuwa wakf kwake kwa kutiwa unajisi.
- 12
- 13 Na hii sheria ya Mnathiri, siku zake za kuwa wakf zilipotimia : ataletwa mlango-
- 14 ni kwa hema ya kusanyiko ; naye atamtolea Bwana matoleo yake, mwana kondoo mume mmoja wa mwaka wa kwanza mkamilifu kwa kafara, na mwana kondoo mke mmoja wa mwaka wa kwanza mkamilifu ya thambi, na kondoo mume mmoja
- 15 mkamilifu za amani, na kikapo cha mikate isiyochachwa, na maandazi ya unga mzuri uliochanganyika na mafuta, na makaki yasiyochachwa, yaliyotiwa mafuta, na sadaka yao ya unga, na mamiminiko yao.
- 16 Naye mkohani ataleta mbele ya Bwana,
- 17 atamtolea ya thambi, na kafara : na yule kondoo mume atamtolea Bwana sadaka ya matoleo ya amani, pamoja na kikapo cha mikate isiyochachwa : mkohani atatoa tena sadaka yake ya unga, na mimi-
- 18 niko lake. Naye Mnathiri atanyoa kitwa cha kuwa wakf kwake mlangoni pa hema ya kusanyiko, na kuzichukua nyele za kitwa cha kuwa wakf kwake, na kutia motoni

- 19 ulioko chini ya sadaka ya matoleo ya amani. Na mkohani atalitwaa bega lililotokota la kondoo mume na moja kati-ka maandazi yasiyochachwa ya kikaponi, na kaki moja lisilochachwa, atayatiamikononi kwa Mnathiri, baada yake akii-
- 20 sha kunyoa cha kuwa wakf kwake: na mkohani atayatikisa tikiso mbele ya Bwana; takatifu hili la mkohani, pamoja na kifua cha kutikisa na paja la kuinua: na baadaye
- 21 ruhusa Mnathiri anywe mvinyo. Hii sheria ya Mnathiri, awekaye nathiri, matoleo yake kwa Bwana kwa kuwa wakf kwake, zayidi ya yale mkono wake uwezayo kuyapata: kwa nathiri yake aliyoiweka, hivi akafanye juu ya sheria ya kuwa wakf kwake.
- 22 Bwana akamwambia Musa akisema,
- 23 Uwaambie Harun na waanawe, ukisema, Hivi mtakavyowabariki waana wa Israeli; mtawaambia,
- 24 Bwana akubariki, akulinde:
- 25 Bwana akutolee nuru ya uso wake, akurehemie:
- 26 Bwana akuinulie uso wake, akupe amani.
- 27 Ndivyo watakavyoliwika jina langu juu ya waana wa Israeli; nami nitawabariki.

SURA 7.

IKAWA siku alipokwisha Musa kupandisha masikani, na kuitia mafuta, na kui-

- takasa, na vyombo vyake vyote, na mathbahu na vyombo vyake vyote, na kuvitia mafuta na kuvitakasa; wakuu wa Israeli, walio juu ya nyumba za baba zao, wakaleta matoleo; hawa wakuu wa makabila, hawa ndio waliowasimamia wale waliohesabiwa: wakamletea Bwana matoleo yao, magari sita yenyi mafuniko, na ng'ombe kumi na wawili: kwa wakuu wawili wawili gari moja moja, na kwa killa mkuu ng'ombe mmoja: wakawatolea mbele ya masikani.
- 4 Bwana akamwambia Musa, akisema, (5) Po-
5 kea kwao, wapate kuwa wa kuhudumia huduma ya hema ya kusanyiko; na utawagawia Walawi, killa mtu kwa huduma yake.
- 6 Musa akayapokea magari na ng'ombe,
7 akawagawia Walawi. Magari mawili na ng'ombe wa'nne akawagawia waana wa
8 Gershon, kwa huduma yao: na magari ma'nne na ng'ombe wanane akawagawia waana wa Merari, kwa huduma yao, chini ya mkono wa Ithamar mwana wa
9 Harun mkohani. Asiwagawie waana wa Kohath: kwa kuwa huduma ya patakatifu
10 kwao; nao huchukua mabegani. Wakuu wakatolea kwa kuwekea wakf mathbahu, siku ilipotiwa mafuta, hatta wakuu wakatoa matoleo yao mbele ya mathbahu.
- 11 Bwana akamwambia Musa, Watatoa matoleo yao, killa mkuu siku yake, kwa kuwekea wakf mathbahu.
- 12 Akawa Nahshon mwana wa Amminadab, wa kabila la Yuda, aliyetoa matoleo yake

- 13 siku ya kwanza: sahani ya fetha moja, uthani mia thelathini, kopo la fetha moja la shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika na mafuta kwa sadaka ya unga;
- 14 mwiko wa thahabu mmoja wa kumi, umejaa uvumba; ndama mmoja, kondoo mume
- 15 mmoja, mwana kondoo mume mmoja wa
- 16 mwaka wa kwanza kwa kafara: beberu
- 17 mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume wa mwaka wa kwanza watano: haya matoleo ya Nahshon mwana wa Amminadab.
- 18 Siku ya pili akatolea Nethanel, mwana
- 19 wa Zuar, mkuu wa Issakar: akatoa matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia thelathini, kopo la fetha moja la shekeli sabwini kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika
- 20 na mafuta kwa sadaka ya unga; mwiko wa thahabu mmoja wa kumi, umejaa uvu-
- 21 mba; ndawa mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja
- 22 wa mwaka wa kwanza, kwa kafara; beberu mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi;
- 23 na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume wa mwaka kwanza watano: haya matoleo yake Nethanel mwana wa Zuar.
- 24 Siku ya tatu mkuu wa waana wa Za-

- 25 bulon Eliab mwana wa Helon; matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia na thelathini, kopo la fetha moja ya shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika na
- 26 mafuta kwa sadaka ya unga; mwiko wa
- 27 thahabu wa kumi, umejaa uvumba; ndama mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja wa mwaka wa kwanza, kwa kafara; beberu mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume wa mwaka wa kwanza watano: haya matoleo yake Eliab mwana wa Helon.
- 30 Siku ya 'nne mkuu wa waana wa Reuben
- 31 Elizur, mwana wa Shedeur; matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia na thelathini, kopo la fetha moja la shekeli sabwini kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika
- 32 na mafuta kwa sadaka ya unga; mwiko wa thahabu mmoja wa kumi, umejaa uvumba; ndama mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja wa mwaka
- 34 wa kwanza kwa kafara; beberu mmoja
- 35 wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume watano wa mwaka wa kwanza; haya matoleo yake Elizur mwana wa Shedeur.

- 36 Siku ya tano mkuu wa waana wa Simeon
 37 Shelumiel mwana wa Zurishaddai : matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia na thelathini, kopo la fetha moja la shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika na mafuta kwa sadaka ya unga; 38 mwiko wa thahabu mmoja wa kuni, umejaa uvumba : ndama mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja wa 40 mwaka wa kwanza, kwa kafara; beberu 41 mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume watano wa mwaka wa kwanza; haya matoleo ya Shelumiel mwana wa Zurishaddai.
- 42 Siku ya sita mkuu wa waana wa Gad
 43 Eliasaf mwana wa Deuel : matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia na thelathini, kopo la fetha la shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika na mafuta 44 kwa sadaka ya unga; mwiko wa thahabu 45 mmoja wa kuni, umejaa uvumba : ndama mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mmoja wa mwaka wa kwanza, kwa 46 kafara : beberu mmoja wa mbuzi kwayo ya 47 thambi: na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo watano wa mwaka wa kwanza : haya matoleo ya Eliasaf mwana wa Deuel.

- 48 Siku ya saba mkuu wa waana wa Efraim,
 49 Elishama mwana wa Ammihud : matoleo
 yake sahani ya fetha moja, uthani wake
 mia na thelathini, kopo la fetha la shekeli
 sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zime-
 jaa zote unga mzuri uliochanganyika na ma-
 50 futa kwa sadaka ya unga; mwiko wa tha-
 habu mmoja wa kumi, umejaa uvumba;
 51 ndama mmoja, kondoo mume mmoja,
 mwana kondoo mmoja wa mwaka wa
 52 kwanza, kwa kafara: beberu mmoja wa
 53 mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu
 ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, ko-
 ndoo waume watano, mbuzi beberu watano,
 waana kondoo watano wa mwaka wa kwa-
 nza: haya matoleo yake Elishama mwana
 wa Ammihud.
- 54 Siku ya nane mkuu wa waana wa Ma-
 nasse, Gamaliel mwana wa Pedazur:
 55 matoleo yake sahani ya fetha moja, utha-
 ni wake mia na thelathini, kopo la fetha
 moja la shekeli sabwini, kwa shekeli ya
 patakatifu; zimejaa zote unga mzuri ulio-
 changanyika na mafuta, kwa sadaka ya
 56 unga; mwiko wa thahabu mmoja wa kumi,
 57 umejaa uvumba; ndama mmoja, kondoo
 mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja
 58 wa mwaka wa kwanza, kwa kafara; beberu
 59 mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa
 thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wa-
 wili, kondoo waume watano, mbuzi beberu
 watano, waana kondoo waume watano wa
 mwaka wa kwanza; haya matoleo ya Ga-

maliel mwana wa Pedazur.

- 60 Siku ya tissia mkuu wa waana wa Be-
 61 nyamin, Abidan mwana wa Gideoni: ma-
 toleo yake sahani ya fetha moja, uthani wa-
 ke mia na thelathini, kopo la fetha moja la
 shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu;
 zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika
 62 na mafuta kwa sadaka ya unga; mwiko wa
 thahabu mmoja wa kumi, umejaa uvumba;
 63 ndama mmoja, kondoo mume mmoja,
 mwana kondoo mume mmoja wa mwaka
 64 wa kwanza kwa kafara; beberu mmoja wa
 65 mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu
 ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili,
 kondoo waume watano, mbuzi beberu wa-
 tano, na waana kondoo waume watano
 wa mwaka wa kwanza: haya matoleo ya
 Abidan mwana wa Gideoni.
- 66 Siku ya kumi mkuu wa waana wa Dan,
 67 Ahiezer mwana wa Ammi-shaddai: mato-
 leo yake sahani ya fetha moja, uthani wake
 mia na thelathini, kopo la fetha moja la
 shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu;
 zimejaa zote unga mzuri uliochanga-
 nyika na mafuta kwa sadaka ya unga;
 68 mwiko wa thahabu mmoja wa kumi,
 69 umejaa uvumba; ndama mmoja, kondoo
 mumemmoja, mwana kondoo mume mmo-
 ja wa mwaka wa kwanza, kwa kafara;
 70 beberu mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi;
 71 na kwa thabihu ya matoleo ya amani,
 ng'ombe wawili, kondoo waume watano,
 mbuzi beberu watano, waana kondoo wau-

me watano wa mwaka wa kwanza; haya matoleo ya Ahiezer mwana wa Ammi-shaddai.

72 Siku ya edashara, mkuu wa waana wa

73 Ashér, Pagiél mwana wa Okran : matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia na thelathini, kopo la fetha moja la shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika na mafuta kwa sadaka ya unga;

74 mwiko wa thahabu mmoja wa kumi, ume-

75 jaa uvumba; ndama mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja wa

76 mwaka wa kwanza; kwa kafara; beberu

77 mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume watano wa mwaka wa kwanza : haya matoleo yake Pagiél mwana wa Okran.

78 Siku ya thenashara mkuu wa waana

79 wa Naftali, Ahira mwana wa Enan; matoleo yake sahani ya fetha moja, uthani wake mia na thelathini, kopo la fetha moja la shekeli sabwini, kwa shekeli ya patakatifu; zimejaa zote unga mzuri uliochanganyika na mafuta kwa sadaka ya unga;

80 mwiko wa thahabu mmoja wa kumi, ume-

81 jaa uvumba; ndama mmoja, kondoo mume mmoja, mwana kondoo mume mmoja wa

82 mwaka wa kwanza, kwa kafara; beberu

83 mmoja wa mbuzi kwayo ya thambi; na kwa thabihu ya matoleo ya amani, ng'ombe

wawili, kondoo waume watano, mbuzi beberu watano, waana kondoo waume watano wa mwaka wa kwanza; haya matoleo ya Ahira mwana wa Enan.

- 84 Hivi kuweka wakf kwa mathbahu, siku ilipotiwa mafuta, kwa wakuu wa Israeli: sahani kumi na mbili za fetha, makopo kumi na mawili ya fetha, miiko kumi na miwili ya
- 85 thahabu: killa sahani ya fetha ya mia na thelathini, na killa kopo la sabwini: fetha yote ya vyombo elfeen na mia 'nne, kwa
- 86 shekeli ya patakatifu: miiko ya thahabu kumi na miwili imejaa uvumba, kumi kumi kwa shekeli ya patakatifu; thahabu
- 87 yote ya miiko mia na ashariini: nyama zote za kafara ng'ombe kumi na wawili, kondoo waume kumi na wawili, waana kondoo waume wa mwaka wa kwanza kumi na wawili, na sadaka yao ya unga: na beberu wa mbuzi kwayo ya thambi kumi na wawili:
- 88 na nyama zote za thabihu ya matoleo ya amani ng'ombe asharini na wa'nne, kondoo waume settini, mbuzi beberu settini, waana kondoo waume wa mwaka wa kwanza settini. Hivi kuweka wakf kwa ma-
- 89 thabahu, baada ya kutiwa mafuta. Naye Musa alipoingia hemani mwa kusanyiko, asemi naye, ndipo alipoisikia Sauti ikisema naye toka juu ya kisetiri kilichokuwa juu ya sanduku ya ushahidi, toka kati ya makerubi mawili: akasema naye.

SURA 8.

- B**WANA akamwambia Musa, akisema,
 (2) Umwambie Harun, ukaseme naye,
 Utakapowasha taa, taa saba zitaangaza
 3 mbele ya kinara. Akafanya Harun hivi;
 akawasha taa zake mbele ya kinara, kama
 4 Bwana alivyomwamuru Musa. Na hii ka-
 zi yake kinara, thahabu iliyofuliwa: hatta
 kwa shina lake, kwa maua yake, kazi iliyo-
 fuliwa: kwa namna Bwana aliyomwonyesha
 Musa, ndivyo alivyofanya kinara.
- 5 Bwana akamwambia Musa, akisema,
 6 Uwatwae Walawi katika kati ya waana wa
 7 Israeli, ukawatakase. Na haya utakayo-
 watendea, kuwatakasa: uwamiminie maji
 ya kwa thambi, wakapishe wembe juu ya
 mwili wao wote, wakafue nguo zao, wakaji-
 8 takase. Wakatwae ndama, na sadaka ya-
 ke ya unga, unga mzuri uliochanganyika
 na mafuta, na ndama mwingine utatwaa
 9 kwayo ya thambi. Nawe utawatoa Wala-
 wi mbele ya hema ya kusanyiko: na-
 we utawakusanya kusanyiko lote la waana
 10 wa Israeli: nawe utawatoa Walawi mbele
 ya Bwana: na waana wa Israeli watawa-
 11 wekea Walawi mikono yao: na Harun ata-
 watoa Walawi mbele ya Bwana kwa tikiso,
 kwa ajili ya waana wa Israeli, wawe wa
 12 kuhudumia huduma yake Bwana. Nao
 Walawi wataweka mikono vitwani kwa
 ng'ombe: nawe umtoe mmoja kwayo ya
 thambi, na wa pili kafara, kwa Bwana, ku-

- 13 wafanyia upatanisho Walawi. Nawe utawaweka Walawi inbele ya Harun, na mbele ya waanawe, utawatoa tikiso kwa
- 14 Bwana. Ndivyo utakavyowatenga Walawi katika kati ya waana wa Israeli, na
- 15 lawi watakuwa wangu. Na baadaye Walawi wataingia kuihudumia hema ya kusanyiko : nawe utawatakasa, na kuwatoa kwa
- 16 tikiso. Kwani kupewa nimepewa hawa katika kati ya waana wa Israeli; mahali pao wote wafunguao tumbo la mama, hatta wazaliwa wa kwanza wa waana wa Israeli
- 17 wote, nimewatwalia hawa. Kwani wazaliwa wa kwanza wote katika waana wa Israeli wangu, wa waana Adamu na wa nyama : siku ile nilipowapiga wazaliwa wa kwanza wote katika inchi ya Misri naliwatakasa
- 18 kwangu mwenyewe. Nami nimewatwaa Walawi mahali pa wazaliwa wa kwanza
- 19 wote kati ya waana wa Israeli. Tena Walawi kupewa amepewa nami Harun na waanawe katika waana wa Israeli, kuhudumia huduma ya waana wa Israeli katika hema ya kusanyiko, na kuwafanyia upatanisho waana wa Israeli : isiwe tauni kati ya waana wa Israeli, wakikaribia waana wa
- 20 Israeli kwa patakatifu. Hivi Musa na Harun na kusanyiko lote la waana wa Israeli wakawatendea Walawi : kwa yote Bwana aliyomwamuru Musa juu ya Walawi, ndivyo waana wa Israeli walivyowatendea.
- 21 Walawi wakajitolea ya thambi, wakafusanguo zao; Harun akawatoa kwa tikiso

- mbele ya Bwana ; Harun akawafanyia upa-
 22 tanisho kuwatakasa. Baadaye waliingia
 Walawi kuhudumia huduma yao hemani
 mwa kusanyiko mbele ya Harun, na mbele
 ya waanawe : kama Bwana alivyomwa-
 muru Musa juu ya Walawi, ndivyo walivyo-
 watendea.
- 23 Bwana akamwambia Musa, akisema,
 24 Kwao Walawi haya : wenyi miaka hamsi
 u asharini na zayidi wataingia kungojea
 serikari katika huduma ya hemani mwa
 25 kusanyiko : na wenyi miaka hamsini wata-
 rudi katika kungojea serikari ya huduma,
 26 wala hawatahudumia tena ; lakini watango-
 jea pamoja na ndugu zao katika hema ya
 kusanyiko, kulinda malinzi, na huduma
 wasihudumie. Ndivyo utakavyowatendea
 Walawi kwa malinzi yao.

SURA 9.

- B**WANA akamwambia Musa katika bara
 ya Sinai, mwezi wa kwanza wa mwaka
 wa pili, baada ya kutoka inchi ya Misri,
 2 akisema, Tena waana wa Israeli waifa-
 3 nye pasaka kwa muhulla wake. Siku
 ya arobatashara ya mwezi huu, kati ya
 jioni mbili, mtaifanya kwa muhulla wake :
 kwa sheria zake zote, na kwa maagizo ya-
 4 ke yote mtaifanya. Musa akawaambia
 5 waana wa Israeli, waifanye pasaka. Wa-
 kaifanya pasaka, wa kwanza, siku ya aro-
 batashara ya mwezi, kati ya jioni mbili

- katika bara ya Sinai : kwa yote Bwana aliyomwamuru Musa, ndivyo waliyoyafanya
- 6 waana wa Israeli. Palikuwa na watu, waliokuwa na unajisi kwa mayiti ya mtu, hivi wasiweze kuifanya pasaka siku ile : wakaja mbele ya Musa na mbele ya Harun
- 7 siku ile : na wale watu wakamwambia, Sisi tumetiwa unajisi kwa mayiti ya mtu : kwani tumezuiwa tusitoe matoleo ya Bwana kwa muhulla wake kati ya waana wa Israeli ?
- 8 Musa akawaambia, Ngojeni ; nipate kusikia atakayoamuru Bwana juu yenu.
- 9 Bwana akamwambia Musa, akisema,
- 10 Uwaambie waana wa Israeli, ukisema, kama mtu wenu ao wa vizazi vyenu atakuwa na unajisi kwa mayiti, ao akiwa anasafiri mbali, atamfanyia Bwana pasaka lakini :
- 11 Mwezi wa pili, siku ya arobatashara, wataifanya kati ya jioni mbili : wataila pamoja na mikate isiyochachwa na machungu :
- 12 wasisaze kitu hatta assubuhi, wala kuvunja mfupa wake : kwa sheria yote ya pasaka
- 13 wataifanya. Lakini mtu aliye safi, asiye anasafiri, akiacha kufanya pasaka, roho ile itakatika katika watu wake : kwa saba bu matoleo ya Bwana hakumtolea kwa muhulla wake, mtu yule ataichukua thambi yake. Na kama mgeni akikaa mweni, atamfanyia Bwana pasaka ; kwa sheria ya pasaka, na kwa maagizo yake, ndivyo atakavyofanya : mtakuwa na sheria moja ya mgeni, na yake mzalia wa inchi.
- 15 Na siku ilipopandishwa masikani wingu

- likafunikiza masikani, hatta hema ya ushahidi : likawako juu ya masikani jioni kama kuonekana kwa moto hatta assubuhi.
- 16 Ndivyo ilivyokuwa dayima : wingu likaifunikiza, na kuonekana kwa moto usiku.
- 17 Na killa lilipoinuliwa wingu katika juu ya ile Hema, halafu yake ndipo wakasafiri waana wa Israeli : na pahali lilipokaa wingu,
- 18 ndipo walipotua waana wa Israeli. Kwa amri ya Bwana waana wa Israeli wakasafiri, na kwa amri ya Bwana wakatua : siku zote wingu lilipokaa juu ya masikani wakawa
- 19 wametua. Na wingu lilipokawia juu ya masikani siku nyingi, ndipo waana wa Israeli wakalinda maliuzi ya Bwana, wasisafiri.
- 20 Marra likiwa wingu siku chache juu ya masikani ; ndipo kwa amri ya Bwana wakatua, na kwa amri ya Bwana wakasafiri.
- 21 Marra wingu likawako tangu jioni hatta assubuhi ; na wingu lilipoinuliwa assubuhi, wakasafiri : ao mchana na usiku, liliponiuli-
- 22 wa wingu wakasafiri. Ka n siku mbili, ao mwezi, ao mwaka, wingu lilipokawia juu ya masikani, likikaa juu yake, waana wa Israeli wakatua, wasisafiri : lakini lilipoinuliwa
- 23 wakasafiri. Kwa amri ya Bwana wakatua, na kwa amri ya Bwana wakasafiri : waka-
yalinda malinzi ya Bwana kwa amri ya Bwana mkononi kwa Musa.

SURA 10.

- 2 **B**WANA akamwambia Musa, akisema,
 3 Ujifanyizie paanda mbili za fetha;
 4 za iliyofuliwa utazifanyiza, nazo zitakuwa
 5 kwako za kuwaitia kusanyiko na kwa sa-
 6 fari ya matuo. Na watakapozipiga, kusa-
 7 nyiko lote watakusanyika kwako mlango-
 8 ni pa hema ya kusanyiko. Na wakipiga
 9 moja tu, ndipo wakuu, walio juu ya elfu
 10 za Israeli, watakusanyika kwako. Na
 11 mtakapopiga mbiu, matuo yaliyoko kwa
 12 mashariki watashika njia. Na mkipiga
 13 mbiu marra ya pili, matuo yaliyoko kwa
 14 kusini watashika njia: watapiga mbiu kwa
 15 safari zao. Lakini kusanyiko litakapoku-
 16 sanyika, mtapiga, wala si kwa mbiu. Na
 17 waana wa Harun, wakohani, watapiga kwa
 18 mapaanda; nazo zitakuwa kwa amri kwe-
 19 nu milele katika vizazi vyenu. Nanyi mta-
 20 kapokwenda vitani katika inchi yenu juu
 21 ya adui awaoneaye, ndipo mtapiga mbiu
 22 na mapaanda; nanyi mtakumbukwa mbele
 23 ya Bwana Muungu wenu, nanyi mtaokoka
 24 katika adui zenu. Tena siku ya furaha
 25 yenu, na siku kuu zenu, na mianzo ya mie-
 26 zi kwenu, mtapiga paanda juu ya kafara
 27 zenu, na juu ya thabihu zenu za matoleo
 28 ya amani; nazo zitakuwa kwenu kwa uku-
 29 mbusho mbele ya Muungu wenu: Mimi
 30 Bwana Muungu wenu.
- 11 Ikawa mwaka wa pili, mwezi wa pili.
 siku ya asharini ya mwezi, wingu likainu-

- liwa katika juu ya masikani ya ushahidi.
- 12 Waana wa Israeli wakashika njia kwa safari zao kutoka bara ya Sinai; wingu likakaa kwa bara ya Paran. Nao kwanza wakashika njia kwa amri ya Bwana mkononi kwa Musa. Na ya kwanza kushika njia bandera ya matuo ya waana wa Yuda kwa majeshi yao: na juu ya jeshi lake
- 15 Nahshon mwana wa Amminadab. Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Issakar
- 16 Nethanel mwana wa Zuar. Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Zebulon Eliab
- 17 mwana wa Helon. Masikani ikashushwa; wakashika njia waana wa Gershon na waana wa Merari, waliochukua masikani.
- 18 Ikashika njia bandera ya matuo ya Reuben kwa majeshi yao: na juu ya jeshi lake
- 19 Elizur mwana wa Shedeur. Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Simeon Shelumiel mwana wa Zurishaddai. Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Gad Eliasaf
- 21 mwana wa Deuel. Na Wakohathi wakashika njia, wakichukua Patakatifu: *wote* wakaipandisha masikani kabla hawajaja.
- 22 Ikashika njia bandera ya matuo ya waana wa Efraim kwa majeshi yao: na juu ya jeshi lake Elishama mwana wa Ammihud.
- 23 Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Manasse Gamaliel mwana wa Pedazur.
- 24 Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Benjamin Abidan mwana wa Gideoni.
- 25 Ikashika njia bandera ya matuo ya waana wa Dan, yaliyo ya kuwakusanya katika ma-

tuo yote, kwa majeshi yao, na juu ya jeshi lake Ahiezer mwana wa Ammishaddai.

- 26 Na juu ya jeshi la kabila la waana wa
 27 Asher Pagiél mwana wa Okran. Na juu ya jeshi la kabila la waana wa Naftali
 28 Ahira mwana wa Enan. Ndivyo walivyo-safiri waana wa Israeli kwa majeshi yao; wakashika njia.
- 29 Musa akamwambia Hobab, mwana wa Reuel Mmidiani, mkwewe Musa, Tunasafiri hatta mahali alipotuambia Bwana, Nita-wapa ninyi: Uje naswi, naswi tutakute-ndea mema: kwani Bwana amenena mema juu ya Israeli. Akamwambia, Siendi; illa kwa inchi yangu na kwa jamaa zangu
 31 nitakwenda. Akasema, Usituache, naku-sihi; ukiwa umejua tutueje katika nyika, nawe utakuwa kwetu mahali pa macho.
 32 Na itakuwa, ukienda naswi, hatta itakuwa, mema yo yote atakayotutendea Bwana, tutakutendea yale yale.
- 33 Wakashika njia toka mlima wa Bwana safari ya siku tatu; likawatangulia sanduku la agano la Bwana safari ya siku tatu,
 34 kuwatafutia pa kupumzikia. Na wingu la Bwana juu yao mchana, walipotoka matuoni.
- 35 Ikawa, sanduku liliposhika njia, Musa husema, Uondoke, Ee Bwana, na adui zako watawanyike; nao wakuchukiao wakimbie
 36 mbele zako. Na lilipostarehe, akasema, Urudi, Ee Bwana, kwa elfu kumi za elfu za Israeli.

SURA 11.

WAKAWA watu wamenung'unikia vi-
 baya msikioni mwa Bwana: akasikia
 Bwana, hasira yake ikawaka; moto wa
 Bwana ukawaunguza, ukawateketeza pa-
 2 nde za mwisho za matuo. Watu waka-
 mlilia Musa; Musa akamwomba Bwana,
 3 moto ukakoma. Nao wakapaita pale Ta-
 bera: kwa sababu moto wa Bwana ukawa-
 unguza.
 4 Na mafuasi waliomo mwao wakatamani
 tamaa: na waana wa Israeli nao wakalia-
 lia, wakasema, Nani atakayetupa nyama,
 5 tule? Twakumbuka samaki, tuliokula
 burre katika Misri; matango, na matikiti,
 na machatsiri, na vitunguu, na shumi:
 6 lakini sasa roho zetu zimekauka; hapana
 kitu: hatuna illa hii man tuitazamie.
 7 Nayo man imefanana na mbegu ya gad, na
 kutazamiwa kwake kama kutazamiwa be-
 8 dola. Wakazunguka watu, wakaikusanya,
 wakaisaga kwa mawe, ao kuitwanga kinu-
 ni, wakaitokosa kwa vijungu, wakaifanyi-
 zia mikate: na tamu yake kama mafuta
 9 mapya. Na umande uliposhuka matuoni
 10 usiku, man ikashuka juu yake. Musa aka-
 sikia watu wakilia kwa jamaa zao, killa
 mtu mlangoni pa hema yake: hasira ya
 Bwana ikawaka sana: Musa akakasirika
 11 naye. Musa akamwambia Bwana, Mbona
 umemtendea vibaya mtumwa wako? na
 mbona sikuona kibali machoni pako, kuwe-

- ka juu yangu mzigo wa watu hawa wote ?
- 12 Nimewachukulia mimba watu hawa wote ?
nimewazaa, uniambie mimi, Uwachukue
kifuani kwako, kama baba mnyonyeshaji
amchukuavyo mtoto mnyonya, hatta inchi
- 13 uliyowaapia baba zao ? Nipate wapi nya-
ma ya kuwagawia watu hawa wote ? Kwa-
ni wanililia wakisema, Tupe nyama, tule.
- 14 Mimi siwezi kuwachukua watu hawa wote
peke yangu, kwani vigumu mno kwangu.
- 15 Na kama utanitendea hivi, uniulie mbali,
nakusihi, nikiwa nimeona ukubali macho-
ni pako, nisione mabaya yangu.
- 16 Bwana akamwambia Musa, Nikusanyie
watu sabwini katika wazee wa Israeli, u-
wajuao kuwa wazee wa watu na wenyi
kuwasimamia ; uwalete katika hema ya
kusanyiko, wasimame huko pamoja nawe.
- 17 Nami nitashuka niseme nawe huko : nami
nitatwaa ya roho iliyoko juu yako, nitawa-
tia wao ; nao watachukua mzigo wa watu
- 18 pamoja nawe, usiuchukue peke yako. Uka-
waambie watu, Jitakaseni kabla ya ke-
sho, nanyi mtakula nyama ; kwani mmelia
masikioni mwa Bwana, mkisema, Nani ata-
kayetupa nyama, tule ? kwani heri kwetu
katika Misri : kwa hiyo Bwana atawapa
- 19 nyama, nanyi mtakula. Hamtakula siku
moja, wala siku mbili, wala siku tano, wala
- 20 siku kumi, wala siku asharini ; lakini mwe-
zi mzima, hatta itakapotoka puani mwenu,
nanyi mkinai : kwa sababu mmemkataa
Bwana aliye kati mwenu, mkilia mbele

- yake, mkisema, Kwani tumetoka Misri ?
- 21 Musa akasema, Watu, nilioko kati mwao, elfu sita mia waendao kwa miguu; nawe umesema, Nitawapa nyama, wale mwezi
- 22 mzima. Watachinjiwa kondoo na ng'ombe, kuwatosha? ao samaki zote za baharini watakusanyikiwa, kuwatosha?
- 23 Bwana akamwambia Musa, Mkono wa Bwana umepunguka bassi? Hatta sasa utaona kama neno langu litakufikia, ama
- 24 sivyo. Musa akatoka, akawaambia watu maneno ya Bwana: akakusanya watu sabwini katika wazee wa watu, akawaweka
- 25 kuizunguka Hema. Bwana akashuka winguni, akasema naye, akatwaa ya roho iliyoko juu yake, akawatia wale wazee sabwini: ikawa, roho ilipostarehe juu yao,
- 26 wakatoa unabii, wakakoma. Wakabaki watu wawili matuoni, jina lake mmoja Eldad, na jina lake wa pili Medad: roho ikastarehe juu yao; nao katika wale walioandikwa, wala hawakutoka kwenda Hema-
- 27 ni; wakatoa unabii matuoni. Akakimbia kijana akamwambia Musa, akasema, Eldad
- 28 na Medad watoa unabii matuoni. Na Isa mwana wa Nun, mngoje wake Musa, mmoja wa wateule wake, akajibu akasema,
- 29 Bwanangu Musa, uwakataze. Musa akamwambia, Umekuwa ua uwivu kwa ajili yangu? Laiti watu wote wa Bwana wangekuwa manabii, Bwana angewatia roho
- 30 yake! Musa akaenda zake matuoni, yeye
- 31 na wazee wa Israeli. Upepo ukaendelea

katika Bwana, ukaleta kwale katika bahari, ukaziacha matuoni, kupata kama safari ya siku mzima upande huu na kama safari ya siku mzima upande ule, kuyazunguka matuo, na kama mikono miwili juu usoni pa
32 inchi. Wakaondoka watu mchana ule wote, na usiku ule wote, na siku ya pili yote, wakazikusanya kwale : aliyekusanya kidogo akakusanya homeri kumi : wakazitanda-
33 tanda kwa pande zote za matuo. Ikiwa nyama bado kati ya meno yao, hawajaisha kuitafuna, hasira ya Bwana ikawaka juu ya watu, Bwana akawapiga watu kwa pigo
34 kuu sana. Wakapaita mahali pale Kibroth-hattaava : kwani ndipo walipowazika watu
35 waliotamani. Toka Kibroth-hattaava watu wakasafiri Hazeroth; wakakaa Hazeroth.

SURA 12.

MARYAMU na Harun wakamnenea Musa kwa sababu ya mwanamke Mku-
 shi aliyemwoa : kwani ameo mwanamke
2 Mkushi. Wakasema, Bwana amesema tu kwa Musa peke yake? Wala hakusema tena
3 kwetu? Bwana akayasikia. Na yule mtu Musa wa upole sana, kuwapita watu wote
4 usoni pa inchi. Akasema Bwana ghafula kwa Musa, na kwa Harun, na kwa Maryamu, Njooni, enyi watatu hemani kwa kusanyiko.
5 Wakatoka wale watatu. Akashuka Bwana kwa nguzo ya wingu, akasimama mlangoni mwa Hema, akawaita Harun na Maryamu :

- 6 wakatoka wote wawili. Akasema, Sikieni enyi maneno yangu : akiwapo mwenu nabii, *mini* Bwana nitajijulisha kwake kwa njozi,
- 7 nitasema naye kwa ndoto. Mtumwa wangu Musa sivyoye; katika nyumba yangu
- 8 yote amini huyu : kanwa kwa kanwa nitasema naye, hatta kwa wazi, wala si kwa mafumbo ; na umbo lake Bwana atalitazama ; mbona bassi hamkuogopa kumnenea
- 9 mtumwa wangu, kumnenea Musa ? Hasira ya Bwana ikawaka juu yao ; akaenda zake.
- 10 Likaondoka wingu katika juu ya Hema ; na, tazama, Maryamu mwenyi ukoma, kama theluji : Harun akamwangalia Maryamu,
- 11 na, tazama, mwenyi ukoma. Harun akamwambia Musa, Ee Bwana wangu, usituwekee, nakusihi, thambi, kwa kuwa tumefanya upumbafu, kwa kuwa tumefanya thambi. Asiwe, naomba, kama mfu, mwili wake nussu ameharika, atokapo
- 12 tumboni mwa mamaye. Musa akamlilia Bwana, akisema, Umponye, Ee Muungu,
- 13 nakusihi. Bwana akamwambia Musa, Babaye angalimtemea mate usoni tu, hangaliona hayu siku saba ? Afungwe nje ya matuo siku saba, na halafu yake ataingizwa tena.
- 14 Maryamu akafungwa nje ya matuo siku saba : wala watu hawakusafiri hatta
- 15 Maryamu alipoingizwa tena. Baadaye watu wakasafiri katika Hazeroth, wakatua katika bara ya Paran.

SURA 13.

BWANA akamwambia Musa, akisema,
 (2) Haya, peleka watu waipieleleze
 inchi ya Kanaan, niwapayo waana wa Isra-
 eli: kwa killa kabila la baba zao mtapele-
 ka mtu, killa mmoja mkuu kati mwao.
 3 Musa akawapeleka hawa katika bara ya
 Paran kwa amri ya Bwana: wote wakiwa
 watu walio juu ya waana wa Israeli.
 4 Na haya majina yao: wa kabila la Reuben
 5 Shammua mwana wa Zakkur. Wa kabila
 6 la Simeon Shafat mwana wa Hori. Wa
 kabila la Yuda Kaleb mwana wa Yefunne.
 7 Wa kabila la Issakar, Igal mwana wa Yusuf.
 8 Wa kabila la Ephraim, Hoshea mwana wa
 9 Nun. Wa kabila la Benjamin Palti, mwa-
 10 na wa Rafu. Wa kabila la Zabulon Gadd-
 11 iel mwana wa Sodi. Wa kabila la Yusuf,
 wa kabila la Manasse Gaddi mwana wa Susi.
 12 Wa kabila la Dan, Ammiel mwana wa Ge-
 13 malli. Wa kabila la Asher, Sethur mwa-
 14 na wa Michael. Wa kabila la Naftali
 15 Nahbi mwana wa Vofsi. Wa kabila la
 16 Gad Geuel mwana wa Maki. Haya maji-
 na ya watu aliowapeleka Musa kuipieleleza
 inchi. Musa akamwita Hoshea mwana
 17 wa Nun Isa. Musa akawapeleka kuipiele-
 leza inchi ya Kanaan, akawaambia, Pande-
 18 ni hivi Kusini, mkapande mlimani: mkaita-
 zame inchi, kama nini; na watu wakaamo,
 kama hodari ao thaifu, kama haba ao wi-
 19 ngi: na nini inchi waikaayo, kama njema ao

- mbaya: na miji gani waikaayo, kama ma-
 20 tuoni ao kama ngomeni; Na nini inchi,
 kama ya unono ao ya kukonda, kama iko
 miti ao sivyo. Nanyi mwe hodari, mkalete
 ya matunda ya inchi. Nao wakati wakati
 21 wa malimbuko ya zabibu. Bassi wa-
 kapanda, wakaipieleleza inchi toka bara ya
 Ziu hatta Rehob, hatta kuingilia Hamath.
 22 Wakapanda Kusini, wakatika Hebron: na
 Ahimon, Sheshai na Talmi waana wa
 Anak, *walikuwako*. (Bassi Hebron umeje-
 ngwa miaka saba kabla ya Zoan, ulioko
 23 Misri.) Wakafika kwa boonde ya Eshkol,
 wakakata huko tawi la chana moja ya za-
 biou, wakaichukua kwa gongo kati ya watu
 24 wawili: tena ya kama-manga na tini. Pa-
 kaitwa pale boonde ya Eshkol kwa ile cha-
 na walioikata toka huko waana wa Israeli.
 25 Wakarudi katika kuipieleleza inchi zikiisha
 siku arobaini.
 26 Wakaenda wakamjia Musa, na Harun,
 na kusanyiko lote la waana wa Israeli, kwa
 bara ya Paran, kwa Kadesh, wakawapasha
 habari, wao na kusanyiko lote, wakawao-
 27 nyasha matunda ya inchi. Wakamwambia,
 wakasema, 'Tumefika katika inchi ulikotu-
 peleka, ndiyo ijaayo maziwa na asali; na
 28 haya matunda yake. Lakini watu wakaao
 katika inchi hodari, na miji yenyi maboma,
 mikubwa sana: na tena waana wa Anak
 29 tumewaona huko. Amalek wakaa inchi ya
 kusini; na Mhitti na Myebusi, na Mwamo-
 ri, wakaa milimani: na Mkanaani akaa

- karibu na bahari, na ukingoni mwa Yarde-
 30 ni. Kaleb akawanyamazisha watu mbele ya
 Musa, akasema, Tupande marra, tuimiliki ;
 kwani twaweza marithawa kuishinda.
 31 Lakini watu waliopanda pamoja naye wa-
 kasema, Hatuwezi kupanda juu ya watu ;
 32 kwa kuwa hodari kuliko sisi. Wakatoa
 habari mbaya ya inchi waliyoipeleleza kwa
 waana wa Israeli, wakisema, Inchi tuliyo-
 ipita kuipeleleza inchi iwalayo waikaa; na
 watu wote tuliowaona humo watu warefu
 33 mno. Na huko tukawaona Wanefili waa-
 na wa Anak, wa katika Wanefili ; tukawa
 machoni petu kama mapanzi, ndivyo na
 tulivyokuwa machoni pao.

SURA 14.

- W**AKAPALIZA kusanyiko lote waka.
 toa sauti ; watu wakalia usiku ule-
 2 Wakamnung'unikia Musa na Harun waana
 wa Israeli wote : wakawaambia kusanyiko
 lote, Laiti tungalikufa katika inchi ya
 Misri ! ao laiti tungalikufa katika nyikani
 3 humu ! Na kwa nini atuleta Bwana kai-
 ka inchi hii, tuangamie kwa upnga ?
 Wake wetu na wadogo wetu watakuwa
 mateka. Si heri turudi zetu hatta Misri ?
 4 Wakasemana, Tufanye jemadari, turudi
 5 Misri. Wakaanguka Musa na Harun usoni
 pao mbele ya jamaa yote ya kusanyiko la
 6 waana wa Israeli. Na Isa mwana wa Nun
 na Kaleb mwana wa Jefunne, katika wale

- walioipeleleza inchi, wakararua nguo zao,
 7 wakawaambia kusanyiko lote wa waana wa
 Israeli, wakisema, Inchi tuliyoipita kuipe-
 8 leleza, inchi njema sana sana. Kama Bwana
 akipendezewa naswi, bassi naye atatuleta
 katika inchi hii, atatupa ; inchi ijaayo mazi-
 9 wa na asali. Illa msimwasi Bwana, wala
 msiogope watu wa inchi ; kwani ni chakula
 kwetu : wameondolewa kivuli katika juu
 yao, na Bwana upo naswi : msiwaogope.
 10 Lakini kusanyiko lote wakaamuru kuwatu-
 pia mawe. Ukaonekana utukufu wa Bwa-
 na katika hema ya kusanyiko mbele ya
 waana wa Israeli wote.
- 11 Bwana akamwambia Musa, Hatta lini
 watu hawa watanitharau ? Hatta lini wasi-
 jenisadiki kwa ishara zote nilizotenda kati
 12 mwao. Nitawapiga kwa tauni, nitawao-
 ndoa wasirithi, nawe nitakufanya taifa
 13 kubwa na hodari kuliko wao. Musa aka-
 mwambia Bwana, Bassi Wamisri watasikia ;
 kwani ukawaleta watu hawa kwa uwezo
 14 wako katika kati yao ; Nao watawaambia
 wakaao katika inchi hii : wamesikia kama
 wewe Bwana kati ya watu hawa : kama
 wewe Bwana umeonwa uso kwa uso, na
 wingu lako kuwasimamia, nawe kuwata-
 ngulia, mchana kwa nguzo ya uwingu, na
 15 kwa nguzo ya moto usiku. Bassi ukiwaua
 watu hawa kama mtu mmoja, ndipo mata-
 ifa waliosikia habari zako watasema, waki-
 16 nena, Kwa sababu Bwana hukuweza ku-
 waleta watu hawa katika inchi aliyowaapia,

- 17 kwa hiyo amewaua barani. Bassi, naku-
sihi, sasa uwezo wa Bwana utukuke kama
18 ulivyosema, ukinena, Bwana mvumilivu,
mwingi wa rehema, auachaye uovu na kosa,
wala kuachilia hataachilia ; akipatiliza uovu
wa baba juu ya watoto, na juu ya wa tatu
19 na juu ya wa 'nne. Samehe, nakusihi, uovu
wa watu hawa kwa wingi wa rehema zako,
na kama ulivyowasamehe watu hawa tangu
20 Misri hatta sasa. Bwana akasema, Nime-
21 samehe kwa neno lako : lakini hakika niishi-
vyo, na kama dunia yote itakavyojaa utu-
22 kufu wa Bwana ; kwa sababu watu wale
wote walionona utukufu wangu, na ishara
zangu nilizotenda kwa Misri na katika
jangwa, nao wamenijaribu marra hizi kumi,
23 wala hawakuisikiliza sauti yangu : kweli
hawataiona inchi niliyowaapia baba zao,
wala hawataiona hatta mmoja wao walioni-
24 tharau : lakini mtumwa wangu Kaleb, sa-
babu alikuwa na roho nyingine ndani
yake, naye amenifuata halisi, yeye nitamle-
ta katika inchi aliyoiingia ; na wazao wake
25 wataimiliki. Bassi Mwamaleki, na Mkana-
ani wanakaa kitako boondeni : kesho geu-
keni mkaende zenu barani njia ya Bahari
ya Sham.
- 26 Bwana akamwambia Musa na Harun,
27 akisema, Hatta lini na kusanyiko hili baya,
waninung'unikia? Nimesikia manung'uni-
ko ya waana wa Israeli waninung'unikiayo.
28 Waambieni, Niishivyo, asema Bwana, ka-
ma mlivyosema masikioni mwangu ndivyo

- 29 nitakavyowatendea : mizoga yenu itaanguka barani humu; na wote waliohesabika kwenu, kwa kadri ya hesabu yenu yote, wenyi miaka asharini na zayidi, walioninung'unikia, hakika yenu hamtaingia inchi niliyoinulia mkono wangu, niwakalishe mle, illa Kaleb mwana wa Yefunne, na
- 30 Isa mwana wa Nun. Lakini wadogo wenu, mliowasema, kama watakuwa meteka, wao nitawaingiza, nao watajua inchi mliyoi-
- 32 kashifu. Nanyi mizoga yenu itaanguka
- 33 barani humu. Na watoto wenu watakuwa wachunga barani miaka arobaini, na masherati yenu watayachukua, hatta mizoga
- 34 yenu itakapoangamia barani humu. Kwa hesabu ya siku mlizopelelezea inchi, siku arobaini, kwa killa siku mwake wake, mtayachukua maovu yenu, miaka arobaini,
- 35 nanyi mtajua nilivyofarakana. Mimi, Bwana, nimesema, hakika haya ndiyo nitakavyowatendea kusanyiko hili baya lote, waliokusanyika juu yangu: barani humu
- 36 wataangamia, na huko watakufa. Nao watu aliowapeleka Musa kuipeleleza inchi, waliorudi, na kuwanung'unisha kusanyiko lote juu yake, kwa kutoa habari mbaya ya
- 37 inchi, hatta watu wale walioleta habari mbaya ya inchi, wakafa kwa tauni mbele
- 38 ya Bwana. Lakini Isa mwana wa Nun na Kaleb mwana wa Yefunne wakaishi katika watu wale waliokwenda kuipeleleza
- 39 inchi. Musa akawaambia waana wa Israeli maneno haya yote, wakalia watu sana.

40 Wakaondoka assubuhi mapema, wakapanda juu mlimani, wakisema, Tazameni, sisi, nasi tutapanda mahali, Bwana alipotuahia
 41 dia: kwani tumekosa. Akasema Musa, Kwani nini bassi mwaikhalifu amri ya Bwana,
 42 ikiwa haitafanikiwa. Msipande, kwani Bwana hapo mwenu; msipigwe mbele ya
 43 adui zenu. Kwani huko Mwameleki na Mkanaani mbele yenu, nanyi mtaanguka kwa upanga: kwa sababu mmerudi nyuma katika kumfuata Bwana, kwa hiyo Bwana
 44 hatakuwa pamoja nanyi. Nao wakajitapa kupanda juu mlimani; illa sanduku la agano la Bwana na Musa hawakuondoka matuoni. Bassi wakashuka Mwamaleki, na Mkanaani waliokaa mlimani mle, wakawapiga, wakawaangamiza hatta Horma.

SURA, 15.

BWANA akamwambia Musa, akisema,
 (2) Uwaambie waana wa Israeli, ukaseme nao, Mtakapofika inchini mwa makao
 3 yenu, niwapayo, mtakapomfanyia Bwana sadaka kwa moto, ao kafara, ao thabihu, kwa kuondoa nathiri, ao kwa sadaka ya moyo, ao katika siku kuu zenu kumfanyia Bwana nukato la utulizo, katika ng'ombe
 4 ao katika kondoo: bassi atakayetoa matoleo atamtolea Bwana sadaka ya unga ya sehemu ya kumi ya unga mzuri umechanganyika nayo ya 'nne ya hini ya mafuta:
 5 na mvinyo kwa miminiko, ya 'nne ya hini,

utaifanyizia kafara, ao thabihu, kwa killa
 6 mwana kondoo. Ao kondoo mume, utamfanyizia sadaka ya unga, sehemu za kumi mbili za unga mzuri umechanganyika
 7 na ya tatu ya hini ya mafuta. Na mvinyo kwa miminiko utamtolea Bwana ya tatu
 8 ya hini, nukato la utulizo. Na utakapofanyiza ng'ombe kafara ao thabihu kwa kundoa nathiri, ao thabihu za amani kwa
 9 Bwana, bassi atatoa pamoja na ng'ombe sadaka ya unga ya sehemu za kumi tatu za unga uliochanganyika na nussu ya hini
 10 ya mafuta. Na mvinyo utatoa kwa miminiko nussu ya hini ya mvinyo, kwa sadaka ya moto, nukato la utulizo kwa Bwana.
 11 Ndivyo itakavyofanyika kwa killa ng'ombe, ao kwa killa kondoo mume, ao kwa killa katika waana kondoo waume, ao katika
 12 ka waana mbuzi. Kwa hesabu mtakavyofanyiza, ndivyo mtakavyomfanyia killa
 13 moja kwa hesabu yao. Wazalia wote watafanya haya kwa namna hii, kwa kutoa sadaka ya moto, nukato la utulizo kwa
 14 Bwana. Na kama mgeni akikaa mwenu, ao ye yote kati yenu kwa vizazi vyenu, atataka kutoa sadaka ya moto, nukato la
 15 utulizo kwa Bwana, mfanyavyo ninyi, afanye na yeye. Kwa jamaa agizo moja, kwenu na kwa mgeni akaaye, agizo la
 milele kwa vizazi vyenu: kama ninyi, ndivyo atakavyokuwa mgeni mbele ya Bwana.
 16 Torati moja na sheria moja kwenu na kwa mgeni akaaye mwenu.

17
 18
 19
 20 Y
 21 vy
 ya
 ya
 22
 23 te,
 Bw
 tang
 24 ye
 likit
 chon
 fany
 la ut
 yake
 sheri
 25 tham
 tanish
 eli,
 nao w
 bihu
 26 ya Bw
 te la
 naye
 27 kukos
 mmoja
 atatoa
 28 wa kw

- 17 Bwana akamwambia Musa, akisema,
18 Uwaambie waana wa Israeli, ukaseme nao,
19 Mtakapoingia inchi niwapelekako, bassi
itakuwa, mtakapokula mikate ya inchi,
mtamtolea Bwana thabihu ya kuinua.
20 Ya kwanza ya mseto wenu mtatoa mkate
wa kuinua: kama ya kuinua ya sakafu ndi-
21 vyo mtakavyoiinua. Katika ya kwanza
ya mseto wenu mtamtolea Bwana thabihu
ya kuinua katika vizazi vyenu.
22 Na mtakapokosa, msitende amri hizi zo-
23 te, Bwana alizomwambia Musa, hatta yote
Bwana aliyowaamuru kwa mkono wa Musa,
tangu siku Bwana alipotoa amri na baada-
24 ye katika vizazi vyenu; bassi itakuwa,
likitendeka neno kwa kukosa, wala si ma-
choni pa kusanyiko, kusanyiko lote wata-
fanya kafara ndama mmoja kwa nukato
la utulizo kwa Bwana, pamoja na sadaka
yake ya unga, na miminiko lake, kwa
sheria, na mbuzi mume mmoja sadaka ya
25 thambi. Naye mkohani atawafanyia upa-
tanisho kusanyiko lote la waana wa Isra-
eli, nao watasamehewa; kwa kuwa kosa,
nao wamemletea Bwana matoleo yao, tha-
bihi kwa moto, nayo ya thambi yao mbele
26 ya Bwana kwa kosa lao: na kusanyiko lo-
te la waana wa Israeli watasamehewa,
naye mgeni akaaye mwao; kwani kwa
27 kukosa kwao watu wote. Na kama mtu
mmoja afanya thambi kwa kukosa, bassi,
atatoa ya thambi mbuzi mke wa mwaka
28 wa kwanza. Naye mkohani atamfanyia

- upatanisho roho yenyi kukosa, afanyaye thambi kwa kukosa, mbele ya Bwana, kumfanyia upatanisho; naye atasamehewa.
- 29 Mzalia wa waana wa Israeli, na mgeni akaaye mwao, sheria moja kwao wakitenda
- 30 kwa kukosa. Lakini roho atendaye kwa mkono wa juu, akiwa mzalia ao mgeni, huyu amshutumtu Bwana; na roho ile ita-
- 31 katika katika watu wake. Kwa kuwa ametharau neno la Bwana, na kukhalifu amri yake; roho ile itakatika kabisa, uovu wake utakuwa juu yake.
- 32 Na waana wa Israeli walipokuwako barani, walimwona mtu anaokota kuni siku
- 33 ya sabato. Nao waliomwona anaokota kuni wakamleta kwa Musa na kwa Harun, na
- 34 kwa kusanyiko lote. Wakamtia kulindwa, kwa sababu hayakuthihirika atakayotenda.
- 35 Bwana akamwambia Musa, Ku-uawa atauawa huyu: kusanyiko lote wata-
- 36 mtupia mawe nje ya matuo. Wakamtoa kusanyiko lote nje ya matuo, wakamtupia mawe akafa; Bwana alivyomwamuru Musa.
- 37 Bwana akamwambia Musa, akisema,
- 38 Uwaambie waana wa Israeli, ukawaamuru, wajifanyizie matamvua katika pindo za nguo zao vizazi vyao vyote, nao wazitie ma-
- 39 tamvua za killa upindo kamba ya samawati: nayo itakuwa kwenu kwa matamvua, mpatete kutazama; na kukumbuka amri zote za Bwana, na kuzifanya; msichungulie kwa moyo wenu wenyewe na kwa macho yenu
- 40 wenyewe, mlivyozoea kufanya asharati

nayo: nanyi mkumbuke, mzitende amri zangu zote, na kuwa watakatifu kwa Muungu wenu. Mimi Bwana Muungu wenu, niliyewaleta katika inchi ya Misri, kuwa Mutingtu wenu: mimi Bwana Muungu wenu.

SURA 16.

A KATWAA *watu* Kora mwana wa Izhar mwana wa Kohath, mwana wa Lawi, na Dathan na Abiram, waana wa Eliab, na On, mwana wa Peleth, waana wa Reuben, 2 wakaondoka mbele ya Musa, na watu wa waana wa Israeli, miteen na hamsini wakuu wa jamaa, wateule wa kusanyiko, watu wenyi sifa: wakakusanyika juu ya Musa na juu ya Harun, wakawaambia, Yatosha kwenu, wakiwa watakatifu jamaa yote, killa mmoja wao, naye Bwana kati mwao: mbona bassi mwajivuna juu ya kusanyiko la Bwana? 4 Akasikia Musa akaanguka usoni pake: 5 akamwambia Kora na makutano yake yote, akisema, Assubuhi Bwana ataonyesha nani wake, na nani mtakatifu, na nani atakayemkaribisha kwake, hatta atakayemchagua atamkaribisha kwake. Fanyeni hivi; twaeni vyetezo, Kora na makutano 7 yake yote; vitieni moto, mkaviweke vukizo mbele ya Bwana kesho: na itakuwa mtu Bwana atakayemchagua, yeye mtakatifu: 8 yatosha kwenu, enyi waana wa Lawi. Musa

- akamwambia Kora, Sikieni sasa, enyi waa-
 9 na wa Lawi: Kidogo kwenu, ya kuwa
 Muungu wa Israeli amewatenga ninyi ka-
 tika makutano ya Israeli, awakaribishe
 ninyi kwake; kuhudumia huduma ya masi-
 kani ya Bwana, na kusimama mbele ya
 10 makutano kuwangojea; na ya kuwa ame-
 kukaribisha wewe na ndugu zako wote
 waana wa Lawi pamoja nawe? mkautafuta
 11 ukohani pia? Kwa hiyo wewe na kusanyi-
 ko lako lote mmekusanyika juu ya Bwana:
 naye Harun, nani yeye mmnung'unikie?
 12 Musa akapeleka kuwaita Dathan na Abi-
 ram, waana wa Eliab: wakasema, Hatuji
 13 juu. Kidogo ya kuwa umetupandisha kati-
 ka inchi ijaayo maziwa na asali, kutua nyi-
 kani, illa kumiliki ujimilikishe juu yetu.
 14 Wala si kwa inchi ijaayo maziwa na asali
 ulikotuleta; ao kutupa milki ya makoonde
 na mizabibu: utawachoma macho hawa?
 15 hatuji juu? Musa akakasirika sana, aka-
 mwambia Bwana, Usiangalie sadaka yao:
 hatta punda mmoja wao sikuwatwalia, wa-
 16 la sikuthulumu mmoja wao. Musa aka-
 mwambia Kora, Uwe wewe na makutano
 yako yote mbele ya Bwana, wewe, nao, na
 17 Harun, kesho: mkatwae killa mtu chetezo
 chake, mkavitie vukizo, mkalete mbele ya
 Bwana killa mtu chetezo chake, vyetezo
 miteen hamsini; wewe pia, na Harun, killa
 18 mmoja na chetezo chake. Wakatwaa killa
 mtu chetezo chake, wakavitia moto waka-
 viwekea vukizo, wakasimama mlangoni pa

- hema ya kusanyiko pamoja na Musa na
 19 Harun. Kora akakusanya juu yao maku-
 tano yote mlangoni pa hema ya kusanyiko :
 ukaonekana utukufu wa Bwana kwa ma-
 kutano yote.
- 20 Bwana akawaambia Musa na Harun, a-
 21 kisema, Jitengeni katika kati ya maku-
 tano haya, nipate kuwateketeza marra
 22 moja. Wakaanguka usoni pao, wakasema,
 Ee Muungu, Muungu wa roho za mwili
 wote, mtu mmoja atafanya thambi, nawe
 23 utaghathabikia makutano yote? Bwana
 24 akamwambia Musa, akisema, Uwaambie
 makutano ukisema, Ondokeni katika kari-
 bu ya masikani ya Kora na Dathan na
 25 Abiram. Akasimama Musa akaenda kwa
 Dathan na Abiram; wakamfuata wazee
 26 wa Israeli. Akawaambia makutano, akise-
 ma, Ondokeni, nawasihi, katika hema za
 watu hawa wabaya, wala msiguse cho chote
 kilicho chao msipotee katika thambi zao
 27 zote. Bassi wakapanda katika masikani ya
 Kora, na Dathan, na Abiram, pande zote ;
 wakatoka Dathan na Abiram, wakasimama
 mlangoni pa hema zao, na wake wao, na
 28 waana wao, na wadogo wao. Musa akase-
 ma, Kwa hiyo, mtajua kama Bwana ameni-
 peleka nifanye kazi hizi zote ; kwani si kwa
 29 nia yangu mwenyewe. Kama kwa kufa kwa
 ki-mwana-Adamu watakufa hawa, ao kama
 kwa kujiliwa kwa kimwana-Adamu wataji-
 liwa hawa ; Bwana hakunipeleka mimi
 30 bassi. Lakini kama Bwana ataumba umbo,

- na inchi itafumbua kinwa chake, na kuwameza pamoja na vyote vilivyo vyao, nao kushuka wahayi kwa ahera; ndipo mtatambua,
- 31 kama watu hawa wamemtharau Bwana. Ikawa, alipokiisha kusema maneno haya yote,
- 32 inchi ya chini yao ikapasuka: Dunia ikafumbua kinwa chake, ikawameza wao na nyumba zao, na watu wote walio wa Kora na
- 33 mali zao zote. Bassi wakashuka wao, na vyote vilivyo vyao, wahayi kwa ahera: dunia ikawafunika wakapotea katika kati ya
- 34 kusanyiko. Na Waisraeli wote wa pande zao wakakimbia kwa kilio chao: kwani waka-
- 35 sema, Dunia isitumeze sisi. Moto ukatoka kwa Bwana, ukawateketeza watu miteen na hamsini waliotoa vukizo.
- 36 Bwana akamwambia Musa, akisema,
- 37 Umwambie Eleazar mwana wa Harun mkohani, aviinue vyetezo kwenyi kuteketeza, ukaumwage moto kule; kwani vita-
- 38 katifu; vyetezo vyao hawa waliofanya thambi juu ya roho zao wenyewe, vikafanyike sahani zilizofuliwa mafuniko ya mathabahu; kwani wamevitoa mbele ya Bwana, navyo vitakatifu: na vitakuwa ishara
- 39 kwa waana wa Israeli. Akavitwaa Eleazar mkohani vyetezo vya shaba, walivyovitoa waliounguzwa; wakavifua mafuniko
- 40 ya mathbahu: ukumbusho kwao waana wa Israeli kwa maana asikaribie mgeni asiye wa wazao wa Harun, kuvukiza vukizo mbele ya Bwana; asiwe kama Kora

na kama makutano yake : Bwana alivyomwambia kwa mkono wa Musa.

- 41 Lakini siku ya pili jamaa yote ya waana wa Israeli wakamnung'unikia Musa na Harun, wakisema, Ndinyi mliowaua watu wa
- 42 Bwana. Ikawa, walipokusanyika jamaa juu ya Musa na juu ya Harun, waliangalia hema ya kusanyiko; na, tazama, wingu likaifunikiza, utukufu wa Bwana ukaonekana. Wakaja Musa na Harun mbele ya hema
- 43 ya kusanyiko. Bwana akamwambia Musa, akisema, Ondokeni katika kati ya jamaa hawa, nipate kuwateketeza marra moja.
- 46 Wakaanguka usoni pao. Musa akamwambia Harun, Twaa chetezo chako, ukakitie moto katika mathbahu, ukakiwekee vukizo, ukaende nacho upesi kwa jamaa, ukawafanyie upatanisho : kwani hasira imetoka katika kwa Bwana; tauni imekwanza.
- 47 Harun akatwaa, kama Musa alivyosema, akakimbia katikati ya kusanyiko; na, tazama, tauni imeanza katika watu : akatia vukizo, akawafanyia watu upatanisho.
- 48 Akasimama kati ya wafu na wahayi; ikazuiwa tauni. Bassi waliokufa kwa tauni elfu arobatashara na mia saba juu yao waliokufa kwa neno la Kora. Harun akamrudia Musa mlangoni pa hema ya kusanyiko; tauni ikazuiwa.

SURA 17.

BWANA akamwambia Musa, akisema,
 (2) Unene na waana wa Israeli, ukapokee kwao fimbo moja kwa killa nyumba ya baba, ya wakuu wao wote kwa nyumba za baba zao, fimbo thenashara, uiandikie fimbo ya killa mtu jina lake. Nawe utaiandikia fimbo ya Lawi jina la Harun: kwani killa mkuu wa nyumba za baba zao na fimbo yake moja. Nawe utaziweka hemani mwa kusanyiko mbele ya ushahidi, nionanapo nanyi. Na itakuwa, mtu nitakayemchagua, fimbo yake itachupuka: nami nitakomesha mbele yangu manung'uniko ya waana wa Israeli wanung'unikayo juu yenu. Musa akawaambia waana wa Israeli, na wakuu wao wote wakampa fimbo, killa mkuu moja kwa nyumba za baba zao, fimbo thenashara: na fimbo ya Harun kati ya fimbo zao. Musa akaziweka fimbo mbele ya Bwana katika hema ya ushahidi. Ikawa siku ya pili, Musa akaingia hemani mwa ushahidi; na, tazama, fimbo ya Harun kwa nyumba ya Lawi imechupuka, imetoa machupuka, imechanua maua, imezaa malozi mabivu. Musa akatoa fimbo zote katika mbele ya Bwana kwa waana wote wa Israeli: wakatazama, wakatwaa killa mtu fimbo yake. Bwana akamwambia Musa, Rudisha fimbo ya Harun mbele ya ushahidi, kuwekwa kwa ishara juu ya waana wa kuasi; upate ku-

- yakomesha manung'uniko yao juu yangu,
 11 wasife. Ndivyo alivyofanya Musa : kama
 Bwana alivyomwamuru, ndivyo alivyo-
 fanya.
- 12 Waana wa Israeli wakamwambia Musa,
 wakisema, Angalia, twaangamia, twapotea,
 13 wote twapotea. Killa akaribiaye, killa
 aikaribiaye masikani ya Bwana, hufa :
 je ? tutaharibika wote ?

SURA 18.

BWANA akamwambia Harun, Wewe na
 waanawo na nyumba ya baba yako
 pamoja nawe mtachukua maovu ya pata-
 katifu : nawe na waanawo pamoja nawe
 2 mtachukua maovu ya ukohani wenu. Na
 ndugu zako tena, kabila la Lawi, jamaa ya
 baba yako, uwakaribishe nawe, wapate
 kuungwa nawe, na kukungojea : lakini
 wewe na waanawo pamoja nawe mbele ya
 3 hema ya kusanyiko. Nao watalinda mali-
 nzi yako, na malinzi ya Hema yote ;
 wasivikaribie tu vyombo vya patakati-
 fu, wala kwa mathbahu, wasife, wala hao,
 4 wala ninyi. Nao wataungwa nawe, na
 kulinda malinzi ya hema ya kusanyiko,
 kwa huduma yote ya Hema : wala ngeni
 5 hatakaribia kwenu. Nanyi mtalinda ma-
 linzi ya patakatifu, na malinzi ya mathba-
 hu : isiwe tena hasira juu ya waana wa
 6 Israeli. Nami, angalia, nimewatwaa ndugu
 zenu Walawi katika kati ya waana Israeli ;

- kupewa mmepewa kwa Bwana kuihudumia
 7 huduma ya hema ya kusanyiko. Nawe
 na waanawo pamoja nawe mtalilindia uko-
 hani wenu killa neno la mathbahuni, na
 yaliyomo ndani ya pazia: huduma ya za-
 wadi nimewapa ukohani, na mgeni akari-
 biaye atauawa.
- 8 Bwana akamwambia Harun, Nami, anga-
 lia, nimekupa malinzi ya sadaka zangu
 za kuinuliwa, hatta matakatifu ya waana
 wa Israeli yote nimekupa wewe kwa ajili
 ya kutiwa mafuta, na waanawo, haki ya mi-
 9 lele. Haya yatakuwa yako katika mata-
 katifu ya matakatifu, toka motoni; killa
 matoleo yao, tangu killa sadaka ya unga
 yao, na killa ya thambi yao, na killa ya
 kosa yao, watakayonitolea, takatifu ya mta-
 10 katifu kwako, na kwa waanawo. Kama
 matakatifu ya matakatifu utayala: killa
 mume atayala; yatakuwa matakatifu kwa-
 11 ko. Na haya yako: sadaka ya kuinuliwa ya
 zawadi yao, hatta za kutikisika zote za
 waana wa Israeli; nimekupa wewe na wa-
 anawo na binti zako pamoja nawe, haki
 ya milele. Killa aliye safi nyumbani
 12 mwako atakula. Killa yaliyo manono
 ya mafuta, na yaliyo manono ya zabibu,
 na ya nafaka, ya kwanza yao wampayo
 13 Bwana, umepewa wewe. Malimbuko yo
 yote yaliyomo inchini mwao, wamletayo
 Bwana, yatakuwa yako; killa aliye safi
 14 nyumbani kwako atayala. Killa kilichowe-
 kwa wakf katika Israeli kitakuwa chako.

- 15 Killa afunguaye tumbo la mama, katika nyama yote watakayomtolea Bwana, na wa watu na wa wanyama, atakuwa wako: illa mzaliwa wa kwanza wa watu utamkomboa yakini, na mzaliwa wa kwanza
- 16 wa nyama wasio safi utamkomboa. Nao watakaokombolewa wao wenyi mwezi mmoja utawakomboa, kwa hesabu yako, na fetha ya shekeli tano, kwa shekeli ya
- 17 patakatifu, (nayo gera asharini.) Lakini mzaliwa wa kwanza wa ng'ombe, ao mzaliwa wa kwanza wa kondoo, ao mzaliwa wa kwanza wa mbuzi, usiwakomboe; watakatifu hawa: utainyunyiza damu yao mathbahuni, na shahamu yao utaiteketeza sadaka kwa moto, kuwa nukato la utulizo kwa
- 18 Bwana. Na nyama yao itakuwa yako, kama kifua cha kutikisika na bega la kuu-
- 19 me, itakuwa yako. Sadaka zote za kuinuliwa za matakatifu, waana wa Israeli watakaomtolea Bwana, nimekupa wewe na waanawo na binti zako pamoja nawe, haki ya milele: agano la chumvi hili mbele ya Bwana milele kwako na wazao wako pamoja nawe. Bwana akamwambia Harun,
- 20 Katika inchi yao hutakuwa na milki, wala hutakuwa na sehemu kati mwao: Mimi sehemu yako na milki yako kati ya waana
- 21 wa Israeli. Nao waana wa Lawi, tazama, badala ya zaka zote za Israeli kuwa milki, nimewapa huduma yao wahudumiayo, hu-
- 22 duma ya hema ya kusanyiko. Wala tangu sasa waana wa Israeli wasiikaribie hema ya

kusanyiko, wasijechukua thambi wafe.

- 23 Lakini Walawi wataihudumia huduma ya hema ya kusanyiko, nao watayachukua maovu yao : sheria ya milele katika vizazi vyenu, na kati ya waana wa Israeli, wasiwe na milki. Kwani zaka za waana wa Israeli, watakazomtolea Bwana sadaka ya kuinuliwa, nimewapa Walawi kuwa milki : kwa hiyo nimewaambia, Kati ya waana wa Israeli wasiwe na milki.
- 25 Bwana akamwambia Musa, akisema,
26 Tena utasema na Walawi, ukiwaambia, Mtakapowatwalia waana wa Israeli zaka nilizowapa ninyi katika hawa kwa milki yenu, mtamtotea Bwana sadaka ya kuinuliwa, zaka ya zaka. Nayo sadaka yenu ya kuinuliwa itahesabika kwenu, kama nafaka ya sakafu, na kama kujaa kwake
27 shinikizo. Ndivyo na ninyi mtakavyomwinulia Bwana sadaka ya kuinuliwa katika zaka zenu zote, mtakazopokea kwa waana wa Israeli ; katika hizo mtampa Harun mkohani ya kuinuliwa ya Bwana.
29 Katika zote mtakazopewa mtamwinulia Bwana ya kuinuliwa yote, ya manono yake
30 yote, kilichotakasika katika yake. Bassi utawaambia, Mtakapoyainua manono yake, watahesabikiwa Walawi kama uzidio wake
31 sakafu, na uzidio wake shinikizo. Nanyi mtayala killa pahali, ninyi na nyumba zenu : thawabu yenu hiyo badala ya huduma
32 yenu hemani mwa kusanyiko. Wala kwa hayo hamtachukua thambi, mkiwa mme-

yainua katika manono yake ; nanyi hamtata unajisi matakatifu ya waana wa Israeli, msife.

SURA 19.

BWANA akawaambia Musa na Harun, akisema, (2) Hii sheria ya torati alioyamuru Bwana, akisema, Uwaambie waana wa Israeli wakuletee ng'ombe mke mwekundu mkamilifu, asiye na kilema, 3 asiyepandiwa kamwe na nira : nanyi mampa Eleazar mkohani, naye atamleta nje kutoka matuoni, na mtu atamchinja mbele 4 ya uso wake : na Eleazar mkohani atatwaa ya damu yake kidoleni, na kunyunyiza ya damu yake kwa mbele ya hema ya kusa- 5 nyiko marra saba : na mtu atamteketeza ng'ombe machoni pake; ngozi yake, na nyama yake, na damu yake, na mavi yake, 6 pamoja atayateketeza : na mkohani atatwaa mti wa mwerezi, na ezobu, na nyekundu, na kutupa kati kati ya kuteketea kwa 7 ng'ombe. Ndipo mkohani atafua nguo zake, na mwili wake ataoga majini, na baadaye kuingia matuoni, naye mkohani 8 atakuwa na uchafu hatta jioni. Naye amteketezaye, atafua nguo zake majini, na mwili wake ataoga majini, naye atakuwa 9 na uchafu hatta jioni. Na mtu aliye safi atazoa majifu ya ng'ombe, atayaweka nje ya matuo katika mahali safi, nao kusanyiko la waana wa Israeli watawekewa kuwa maji ya kujitenga ; sadaka ya thambi

- 10 hii. Naye azoaye majifu ya ng'ombe atafua nguo zake, atakuwa na uchafu hatta jioni: nayo itakuwa kwa waana wa Israeli, na kwa mgeni akaaye kati mwao, kwa sheria ya milele.
- 11 Yeye agusaye mayiti ya mtu yo yote, atakuwa na uchafu siku saba:
- 12 atajitakasa nayo huyu siku ya tatu, hatta siku ya saba atakuwa safi: lakini asipojitakasa siku ya tatu, wala siku ya saba hatakuwa safi.
- 13 Ye yote atakayegusa mayiti ya mtu aliyekufa, asiyejitakasa, hutilia uchafu masikani ya Bwana; na roho ile itakatika katika Israeli; kwa kuwa maji ya kujitenga hayakunyunyizwa juu yake, atakuwa na uchafu; uchafu wake bado juu
- 14 yake. Hii torati mtu akifa hemani; killa aingiaye hemani, na killa aliyomo hemani,
- 15 atakuwa na uchafu siku saba. Na killa chombo kilicho wazi, kisichofungwa na
- 16 kifuniko, *kina* uchafu. Naye yote shambani nje agusaye aliyeuawa na upanga, ao mayiti, ao mfupa wa mtu, ao kaburi,
- 17 atakuwa na uchafu siku saba. Na kwake aliye na uchafu, watatwaa ya mavumbi ya kuteketea kwa sadaka ya thambi, nayo
- 18 yatatiwa maji yaliyo hayi chomboni: na mtu safi atatwaa ezobu, ataichovya majini, na kunyunyiza juu ya hema, na juu ya vyombo vyake vyote, na juu ya watu waliomo, na juu yake aliyegusa mfupa, ao
- 19 aliyeuawa, ao mfu, ao kaburi: na yule safi atamnyunyizia aliye na uchafu siku ya tatu, na siku ya saba: hatta siku ya saba ata-

- mtakasa; naye atafua nguo zake, ataoga
 20 majini, na jioni atasafika. Lakini mtu
 aliye na uchafu, asiyejitakasa, itakati-
 ka roho ile katika kati ya kusanyiko, kwa
 kuwa ameitilia uchafu masikani ya Bwana :
 maji ya kujitenga hayakunyunyizwa juu
 21 yake; yuna uchafu. Nayo itakuwa kwao
 sheria ya milele : naye anyunyizaye maji
 ya kujitenga atafua nguo zake; naye agu-
 saye maji ya kujitenga atakuwa na uchafu
 22 hatta jioni. Na killa agusacho aliye na
 uchafu kitakuwa na uchafu, na nafsi yake
 agusaye atakuwa na uchafu hatta jioni.

SURA 20.

- W**AKAFIKA waana wa Israeli, jamii
 yote, bara ya Zin mwezi wa kwanza :
 watu wakakaa Kadesh; Maryamu akafa
 2 huko, akazikwa huko. Wakawa jamaa
 hawana maji; wakakusanyika juu ya Musa
 3 na juu ya Harun. Wakashindana watu na
 Musa wakasema, kusema, Laiti tungekufa
 walipokufa ndugu zetu mbele ya Bwana!
 4 Na mbona mmeleta kusanyiko la Bwana
 katika bara hii, tufe huko sisi na nyama
 5 zetu? Na mbona mmetupandisha sisi kati-
 ka Misri, kutuleta sisi mahali hapa pabaya?
 si mahali pa mbegu, wala pa tini, wala
 pa mizabibu, wala pa kamamanga; wala
 6 hapana maji ya kunywa. Wakaenda Musa
 na Harun katika usoni pa makutano mla-
 ngoni kwa hema ya kusanyiko, wakaangu-

- ka usoni pao : utukufu wa Bwana ukawato-
 7 kea. Bwana akamwambia Musa, akisema,
 8 Twaa fimbo, ukakusanye makutano, wewe,
 na Harun ndugu yako, mkaseme na mwam-
 mba mbele ya macho yao, utokeze maji ya-
 ke ; nawe utawatolea maji mwambani : ndi-
 vyo utakavyowanyweshwa jamii na nyama
 9 zao. Musa akaitwaa fimbo katika mbele ya
 10 Bwana, kama alivyomwamuru. Musa na
 Harun wakawakusanya kusanyiko mbele
 ya mwamba, akawaambia, Sikieni sasa,
 enyi waasi ; katika mwamba huu tuwato-
 11 kezee maji ? Akainua Musa mkono wake,
 akaupiga mwamba kwa fimbo marra mbili :
 maji yakatoka mengi, wakanywa kusanyi-
 12 ko na nyama zao. Bwana akawaambia
 Musa na Harun, Kwa sababu hamkunia-
 mini mimi, kunitakasa machoni pa waana
 wa Israeli, Kwa hiyo hamtawaleta jamii hii
 13 kwa inchi niliyowapa. Haya maji ya Meri-
 ba ; kwa kuwa waana wa Israeli walishi-
 ndana na Bwana, akatakasika kwao.
 14 Musa akampelekea mfalme wa Edom
 wajumbe katika Kadesh, Ndivyo asema-
 vyo ndugu yako Israeli, Wajua wewe kazi
 15 zote zilizotupata sisi : ginsi walivyoshuka
 baba zetu Misri, tukakaa Misri siku nyi-
 ngi ; wakatutendea mabaya Wamisri sisi
 16 na baba zetu : tukamlilia Bwana, akasikia
 sauti yetu, akapeleka malaika, akatutoa
 katika Misri ; naswi, tazameni, kwa Kadesh,
 mji wa mpakani mwako kwa mwisho :
 17 Haya tukapite kwa inchi yako : hatutapita

- kwa koonde, wala kwa mizabibu, wala hatutakunywa maji ya visima: njia ya mfalme tutaiendelea, tusigeuke kwa mkono wa kuume wala wa kushoto, hatta tuta-
- 18 kapokwisha kupita mpaka wako. Akamwambia Edomi, Hutapita kati yangu,
- 19 nisitoke na upanga juu yako. Wakamwambia waana wa Israeli, Kwa njia kuu tutapanda: naswi tukinywa maji yako, mimi na nyama zangu, ndipo nitakupa thamani yake; niache tu, pasipo neno jingine
- 20 lo lote, kupita kwa miguu yangu. Akasema, Hutapita. Edom wakatoka juu yake na
- 21 watu wengi, na kwa mkono hodari. Hivi akakataa Edom kuwapa Israeli mapito kwa mpaka wake: wakamgeukia mbali Israeli.
- 22 Wakasafiri katika Kadesh: wakafika waana wa Israeli, kusanyiko lote, mlimani
- 23 pa Hor. Bwana akawaambia Musa na Harun mlimani pa Hor, kwa mpaka wa
- 24 inchi ya Edom, akisema, Harun atakusanyika kwa watu wake: kwani hataingia inchi niliyowapa waana wa Israeli, kwa sababu mmeasi juu ya neno langu kwa maji
- 25 ya Meriba. Uwatwae Harun na Eleazar mwanawe, ukawapandishe kwa mlima
- 26 Hor. Umvue Harun nguo zake, kamvike nazo Eleazar mwanawe: na Harun atakusanyika, atakufa kule. Akafanya Musa kama Bwana alivyoamuru; wakapanda mlima Hor machoni pa kusanyiko lote.
- 28 Musa akamvua Harun nguo zake, akamvi-

ka nazo Eleazar mwanawe ; akafa Harun huko juu mlimani : wakashuka mlimani
 29 Musa na Eleazar. Na kusanyiko lote walipoona kama Harun amekufa, wakamlilia Harun siku thelathini, nyumba yote ya Israeli.

SURA 21.

A KASIKIA Mkanaani, mfalme wa Arad, aliyekaa Kusini, kama Israeli anakuja njia ya Atharim ; akapigana na Israeli, akatwaa katika wao wafungwa.
 2 Israeli akamwekea Bwana nathiri, akasema, Kama kutia utawatia watu hawa mikononi mwangu, bassi nitaharibu kabisa miji yao. Bwana akaisikiliza sauti ya Israeli, akawatia Wakanaani ; wakawaharibu kabisa wao na miji yao : likaitwa jina la mahali pale Horma.
 4 Wakasafiri katika mlima Hor njia ya bahari ya Sham, kuizunguka inchi ya Edom : watu wkapungukiwa roho kwa sababu ya njia. Wakasema watu juu ya Muungu na juu ya Musa, Mbona mmetupa ndisha katika Misri kufa jangwani ? kwani hapana chakula, hapana maji ; na roho zetu
 6 zachukia chakula hiki chepesi. Bwana akawapelekea watu nyoka za moto, wakauma watu ; hatta wakafa watu wengi wa
 7 Israeli. Watu wakamjia Musa, wakasema, Tumefanya thambi, kwani tumenena juu ya Bwana, na wewe ; umwombe Bwana,

- atuondolee nyoka. Musa akawaombea
 8 watu. Bwana akamwambia Musa, Ujifa-
 nyie nyoka ya shaba, uitie juu ya mti :
 na itakuwa, killa aliyeumwa, aitazamapo,
 9 ataishi. Musa akafanya nyoka ya shaba,
 akaitia juu ya mti : ikawa, nyoka alipomu-
 ma mtu, akiitazama nyoka ya shaba, hui-
 10 shi. Wakasafiri waana wa Israeli, waka-
 11 tua Oboth. Wakasafiri katika Oboth,
 wakatua Iye-abarim, katika bara iliyoko
 12 mbele ya Moab, litokeako . jua. Toka
 huko wakasafiri, wakatua boondeni mwa
 13 Zered. Toka huko wakasafiri wakatua
 ng'ambo ya Arnon wa barani, utokao mpa-
 kani mwa Waamori : kwani Arnon mpaka
 wa Moab, kati ya Moabi na Waamori.
 14 Kwa hiyo husema katika kitabu cha Vita
 za Bwana,
 Vaheb kwa Sufa,
 Na boonde za Arnon,
 15 Na mashuko ya boonde.
 Yatelemkayo makaoni kwa Ar,
 Yaegemeayo mpakani mwa Moab.
 16 Na toka kule kwa Beer, ndicho kisima
 Bwana alichomwambia Musa, Uwakusanye
 watu, nami nitawapa maji.
 17 Ndipo Israeli wakaimba uimbo huu :
 Uchemke, Ee kisima; mkiimbie :
 18 Kisima, walichochimba wakuu,
 Masheki ya watu walichofukua
 Kwa fimbo, kwa magongo yao.
 19 Na toka bara kwa Mathana : na toka Ma-
 thana kwa Nahaliel : na toka Nahaliel kwa

- 20 Bamoth : na toka Bamoth kwa boonde iliyoko uwandani mwa Moab, hatta juu ya Pisga, utazamao jangwani chini.
- 21 Israeli akapeleka wajumbe kwa Sihon
- 22 mfalme wa Waamori, akisema, Nipite kwa inchi yako : hatutageuka wala kwa koonde, wala kwa mizabibu ; hatutakunywa maji ya visimani : njia ya mfalme tutaiendelea, hatta tutakapokwisha kupita mpaka wako.
- 23 Wala Sihon hakuwapa Israeli mapito kwa mpaka wake : akakusanya Sihon watu wake wote, akatoka juu ya Israeli jangwani, akaja Yahaz : akapigana na Israeli.
- 24 Israeli wakampiga kwa upanga, wakaimiliki inchi yake toka Arnon kwa Yabbok, hatta kwa waana wa Ammon ; kwani mpaka wa waana wa Ammon hodari. Israeli wakatwaa miji hii yote : Israeli wakakaa kwa miji yote ya Waamori, kwa Heshbon,
- 26 na kwa vijiji vyake vyote. Kwani Heshbon mji wa Sihon mfalme wa Waamori, akiwa amepigana juu ya mfalme wa Moab wa zamani, na kutwaa inchi yake yote
- 27 mkononi mwake hatta kwa Arnon. Kwa hiyo wenyi methali husema,
 Njooi Heshon,
 Ujengwe ukatengenezwe mji wa Sihon :
- 28 Kwani moto umetoka Heshbon,
 Ndimi za moto mjini kwa Sihon :
 Umeteketeza Ar wa Moab,
 Mabwana wa vilele vya Arnon.
- 29 Ole wako, Moab !
 Umepotea, Ee taifa la Kemosh :

Ametoa waanawe wakimbizi,
Na binti zake wafungwa,
Kwa Sihon mfalme wa Waamori.

30 Tumewapigia; Heshbon umepotea
hatta kwa Dibon,

Tumewateka hatta kwa Nofa,
Ifikayo kwa Medeba.

31 Wakakaa Israeli katika inchi ya Waamo-
32 ri. Musa akapeleka watu kupeleleza Ya-
zer, wakatwaa miji yake, wakawafukuza

33 Waamori waliokuwamo. Wakageuka wa-
kapanda njia ya Bashan: na Og mfalme
wa Bashan akatoka kwenda juu yao, yeye
na watu wake wote, vitani kwa Edrei.

34 Bwana akamwambia Musa, Usimwogope:
kwani mkononi mwako nimemtia, yeye na
watu wake wote, na inchi yake; nawe
utamtendea kama ulivyomtendea Sihon,
mfalme wa Waamori, aliyekaa Heshbon.

35 Bassi wakampiga yeye na waanawe, na
watu wake wote, hatta hakusaziwa mtu:
wakaimiliki inchi yake.

SURA 22.

WAANA wa Israeli wakasafiri, waka-
tua katika inchi sawa ya Moab,
ng'ambo ya Yardeni, kwa Yeriko.

2 Akaona Balak mwana wa Zippor yote

3 Israeli waliyowatendea Waamori. Akao-
gopa sana Moab kwa watu kwa kuwa we-
ngi: akafathaika Moab kwa ajili ya waana

4 wa Israeli. Moab akawaambia wazee wa

Midiani, Sasa wataramba makutano haya
 killa kilichotuzunguka, kama ng'ombe
 hurambavyo majani ya inchi. Na Balak
 mwana wa Zippor mfalme wa Moab zama-
 5 ni zile. Bassi akapeleka wajumbe kwa
 Balaam mwana wa Beor, katika Pethor,
 ulioko Mtoni, pa inchi ya waana wa watu
 wake, kumwita, wakisema, Angalia, wako
 watu, waliotoka Misri; angalia, wafunika
 uso wa inchi, nao wanakaa upande wangu:
 6 njoo bassi sasa, nakuomba, unilaanie watu
 hawa; kwani hodari hawa kuliko mimi:
 labda nitaweza, tuwapige, nami niwafuku-
 ze katika inchi: kwani najua umbarikiye
 wewe hubarikiwa, na umlaaniye wewe
 7 hulaaniwa. Na wazee wa Moab, na wazee
 wa Midiani wakaenda na kiendea mbago
 mikononi; wakaja kwa Balaam, wakamwa-
 8 mbia maneno ya Balak. Akawaambia,
 Laleni hapa usiku huu, nitawaletea tena
 neno, kama Bwana atakavyoniambia: na
 wakuu wa Moab wakakaa na Balaam.
 9 Muungu akamjia Balaam, akasema, Watu
 10 gani waliopo nawe? Balaam akamwambia
 Muungu, Balak, mwana wa Zippor, mfa-
 lme wa Moab, amewatuma kwangu, *akise-*
 11 *ma*, Angalia, watu waliotoka Misri, wafu-
 nika uso wa inchi: sasa bassi njoo, unila-
 nie hawa; labda nitawaweza kwa kupiga-
 12 na, na kuwafukuza. Muungu akamwambia
 Balaam, Usiende nao; usiwalaani watu:
 13 kwani wamebarikiwa. Balaam akaondoka
 assubuhi, akawaambia wakuu wa Balak,

Nendeni inchini mwenu: kwani Bwana
 14 akataa kuniruhusu niende nanyi. Wakuu
 wa Moab wakaondoka, wakaenda kwa
 Balak, wakasema, Balaam akataa kuja
 15 naswi. Akazidi Balak tena kupeleka wa-
 kuu, wengi, na wenyi heshima kuliko wao.
 16 Wakamjia Balaam, wakamwambia, Ndivyo
 asemavyo Balak mwana wa Zippor, Lisi-
 kuzuie neno, nakuomba, katika kunijia:
 17 kwani kuheshimu nitakuheshimu sana,
 na killa utakavyoniambia nitafanya: njoo
 bassi, nakuomba, unilaanie watu hawa.
 18 Akajibu Balaam akawaambia watumwa
 wa Balak, Kama Balak angenipa nyumba
 yake imejaa fetha na thahabu, siwezi ku-
 pita neno la Bwana Muungu wangu, nifanye
 19 madogo ao makuu. Sasa bassi, nawasihi,
 kaeni hapa tena usiku huu, nijue atakalozidi
 20 kuniambia Bwana. Muungu akamjia Ba-
 laam usiku, akamwambia, Kama watu wa-
 mekuja kukuita, ondoka, ukaende nao;
 lakini neno tu nikuambialo, ndilo utakalo-
 21 fanya. Akaondoka Balaam assubuhi, aka-
 tandika punda wake, akaenda nao wakuu
 22 wa Moab. Hasira ya Muungu ikawaka kwa
 kwenda kwake: akasimama malaika wa
 Bwana njiani ampinge. Akawa amepanda
 punda wake, na watumwa wake wawili na-
 23 ye. Punda akamwona malaika wa Bwana
 akisimama njiani, na upanga wake wazi
 mkononi mwake; punda akaepuka njia-
 ni, akaenda koondeni: Balaam akampi-
 24 ga punda, amgeuzie njiani. Akasimama

malaika wa Bwana njiani kati ya miza-
 bibu, penyi kitalu huku na kitalu hu-
 25 ku. Punda akamwona malaika wa Bwa-
 na, akajisonga ukutani, akauseta mguu wa
 26 Balaam ukutani: akampiga tena. Akazi-
 di kuendelea malaika wa Bwana, akasima-
 ma pembamba, pasipo na njia ya kugeukia
 27 kwa kuume, wala kwa kushoto. Punda
 akamwona malaika wa Bwana, akalala
 chini yake Balaam: hasira yake Balaam
 ikawaka, akampiga punda kwa gongo lake.
 28 Bwana akamfunulia kanwa yule punda,
 akamwambia Balaam, Nimefanyaje kwako,
 29 hatta umenipiga marra hizi tatu? Balaam
 akamwambia punda, Kwa sababu umeni-
 thihaki: laiti ningekuwa na upanga mko-
 30 noni, hatta sasa ningalikuua. Punda aka-
 mwambia Balaam, Si mimi punda wako,
 uliyenipanda maisha yako yote hatta leo?
 kuzoea nimezoea kukufanyia hivi? Aka-
 31 sema, La. Bassi Bwana akamfungulia
 macho Balaam, akamwona malaika wa
 Bwana akisimama njiani, na upanga wake
 wazi mkononi: akainama kitwa, akaanguka
 32 usoni pake. Malaika wa Bwana aka-
 mwambia, Mbona umempiga punda wa-
 ko marra hizi tatu? Angalia, nime-
 toka nikupinge, kwa sababu njia yako
 33 ya kassi mbele yangu: punda akani-
 ona, akageuka mbele yangu marra hizi
 tatu: kama asingaligeuka kwangu hakika
 sasa ningalikuua nawe, na huyu ningali-
 34 mwacha hayi. Balaam akamwambia malai-

ka wa Bwana, Nimekosa : kwani sikujua, kama umesimama juu yangu njiani ; na sasa kama baya machoni pako, nitarudi
 35 kwangu. Malaika wa Bwana akamwambia Balaam, Nenda nao watu : lakini neno tu nitakalokuambia, ndilo utakalosema. Bassi
 36 Balaam akaenda na wakuu wa Balak. Na aliposikia Balak kama Balaam amekuja, akatoka kumlaki hatta Mji wa Moab, ulioko mpakani kwa Arnon, mpakani kwa
 37 mwisho. Balak akamwambia Balaam, Kupeleka sikukupelekea nikuite ? Kwa nini hukunijia ? Kwa kweli siwezi kukuheshimia ? Balaam akamwambia Balak, Tazama, nimekujia : hiatta sasa kuweza ninaweza kumena lo lote ? neno Muungu atakalonitia
 38 kinwani ndilo nitakalolisema. Akaenda Balaam na Balak, wakafika Kiriath-huzoth.
 39 Balak akachinja ng'ombe na kondoo, aka mpelekea Balaam, na wakuu waliopo naye.
 40 Ikawa assubuhi Balak akamtwaa Balaam, akampandisha mahali pa juu pa Baal, toka huko akaona miisho ya watu.

SURA 23.

BALAM akamwambia Balak, Unijengee hapa mathbahu saba, ukaniwekee ng'ombe saba na kondoo waume saba.
 2 Balak akafanya kama Balaam alivyosema ; wakatoa Balak na Balaam mathbahuni
 3 ng'ombe na kondoo mume. Balaam akamwambia Balak, Simama penyi kafara ya-

ko, nami nitakwenda ; labda Bwana atakuja kunilaki : nayo yote atakayoniyesha nitakwambia. Akaenda palipochongoka.

- 4 Muungu akamlaki Balaam ; akamwambia, Nimezitengeneza mathbahu saba, nimetoa ng'ombe na kondoo mume mathbahuni.
- 5 Bwana akatia neno kinwani kwa Balaam, akamwambia, Umrudie Balak, na haya
- 6 utakayosema. Akamrudia, na tazama, amesimama penyi kafara yake, yeye na
- 7 wakuu wote wa Moab. Akatunga methali yake, akasema,

Katika Aram Balak amenileta,
Mfalme wa Moab katika milima ya Mashariki :

Njoo, unilaanie Yakobo,
Njoo, ughathabikie Israeli.

- 8 Nimlaanije, Muungu asiyemlaani ?
Nimghathabikieje, Bwana asiyeghathabika ?

- 9 Kwani toka kilele cha miamba namwona,

Na toka milima namtazama :

Angalieni, watu wakaao peke yao,
Wala kati ya mataifa hawatahesabika.

- 10 Nani awezaye kuhasibu mavumbi ya Yakobo,

Ao kujumlisha robo ya Israeli ?

Nafsi yangu nife kifu chake mwenyi haki,

Na mwisho wangu uwe kama wake !

- 11 Balak akamwambia Balaam, Umenifanyiaje ? Uwalaanie adui zangu nimekutwaa,

- 12 na, tazama, kubariki umewabariki. Aki-
 jibu akasema, Silo anitialo Bwana kinwani
 13 linipasalo kulisema? Balak akamwambia,
 Njoo, nakusihi, nami, panginepo, toka huko
 uwaone; mwisho wao tu utawaona, usiwa-
 14 one wote: unilaanie wao toka huko. Aka-
 mchukua uwandani kwa Zofim, hatta juu
 ya Pisga, akajenga mathbahu saba, akatoa
 ngo'mbe na kondoo mume mathbahuui.
 15 Akamwambia Balak, Simama hapa penyi
 16 kafara yako, nikimlaki mimi kule. Bwana
 akamlaki Balaam, akamtia neno kanwani,
 akasema, Umrudie Balak, na haya utaka-
 17 yosema. Akamjia, na, tazama, amesima-
 ma penyi kafara yake, na wakuu wa Moab
 naye. Balak akamwambia, Alisemaje Bwa-
 18 na? Akatuaga methali yake, akasema,
 Ondoka, Balak, ukasikie;
 Unisikilize, mwana wa Zippor:
 19 Muungu si mtu, aseme uwongo;
 Wala mwana Adamu, ajute:
 Amesema, naye hatafanya?
 Ao amenena, naye hatafikiliza?
 20 Angalia, nimepewa nibariki:
 Amebariki, nisiitangue.
 21 Hakutazama uovu kwa Yakobo,
 Wala hakuona thulumu kwa Israeli:
 Bwana Muungu wake pamoja naye,
 Na shangwi la Mfal ne kati mwao.
 22 Muungu awatoaye katika Misri;
 Kwake nguvu kana za nyati.
 23 Hakika uchawi hapana kwa Yakobo,
 Wala uganga kwa Israeli.

- Hatta sasa watahadithiwa Yakobo na Israeli,
Mambo gani aliyoyatenda Muungu!
- 24 Angalia, watu huondoka kama simba mke,
Kama simba hujiinua:
Hatalala hatta atakapokula mawindo,
Na kunywa damu yao waliouawa.
- 25 Balak akamwambia Balaam, Wala kulaani usiwalaani, wala kubariki usiwabariki.
- 26 Akajibu Balaam akamwambia Balak, Siku kwambia, nikisema, Yote atakayosema
- 27 Bwana, sina buddi kuyatenda. Balak akamwambia Balaam, Njoo sasa, nitakuchukua panginepo; labda itampendeza Muungu,
- 28 unilaanie hao toka huko. Balak akamchukua Balaam hatta juu ya Peor, utazamao
- 29 jangwani chini. Balaam akamwambia Balak, Unijengee hapa mathbahu saba, ukaniwekee hapa ng'ombe saba, na kondoo
- 30 saba. Balak akafanya alivyosema Balaam, akatoa ng'ombe na kondoo mume mathbahuni.

SURA 24.

- N**AYE Balaam alipoona ya kuwa jema machoni pa Bwana kubariki Israeli, hakwenda vile vile kama kwanza apatikane na mambo ya uchawi, akalekeza uso wake
- 2 jangwani. Balaam akainua macho, akaona Israeli wametua kwa makabila yao: roho ya
- 8 Muungu ikamjia. Akatunga methali yake, akasema,

- Anena Balaam mwana wa Beor,
Anena mtu aliyefumbwa jicho:
- 4 Anena asikiaye maneno ya Muungu,
Aonaye njozi yake Mwenyiezi,
Akianguka, na macho yake yamefumbuka:
- 5 Ginsi zilivyo njema hema zako, Ee Yakobo,
Masikani zako, Ee Israeli!
- 6 Kama boonde zimetandwa,
Kama bustani ukingoni mwa mto,
Kama miahali aliyoipanda Bwana,
Kama mierezi kwenyi maji.
- 7 Yatamwagika maji katika ndoo zake,
Na mbegu zake kwenyi maji mengi,
Ataiuliwa kuliko Agag mfalme wake;
Na ufaume wake utatukuzwa.
- 8 Muungu amtoaye katika Misri;
Kwake nguvu kama za nyati:
Atameza mataita adui zake,
Atavunjavunja mifupa yao,
Atawapigapiga kwa mishale yake.
- 9 Akainama, akalala, kama simba,
Na kama simba mke; nani atakayeamsha?
Abarikiwe killa akubarikiye,
Alaaniwe killa akulaaniye.
- 10 Hasira yake Balak ikawaka juu ya Balaam,
akapiga makofi: Balak akamwambia Balaam,
Kuwalaani adui zangu nimekuita, na, tazama,
kubariki umewabariki marra hizi
- 11 tatu. Sasa bassi kimbia kwako mahali pako:
nimesema kuheshimu nikuheshimu;

- lakini, tazama, Bwana anakuzuilia heshima.
- 12 Balaam akamwambia Balak, Nami sikuwambia wajumbe wako ulionipelekea, niki-
- 13 sema, Kama Balak angenipa nyumba yake imejaa fetha na thahabu, siwezi kupita neno la Bwana, nifanye mema ao mabaya kwa nia yangu; atakayosema Bwana ndiyo
- 14 nitakayosema? Hatta sasa, tazama, naenda kwa watu wangu: njoo, nitakushauri watu hawa watakawafanyia watu wako
- 15 siku za mwisho. Akatunga methali yake, akasema,
- Anena Balaam mwana wa Beor,
Anena mtu aliyefumbwa jicho;
- 16 Anena, asikiaye maneno ya Muungu,
Ajuaye maarifa yake aliye juu,
Aonaye njozi yake Mwe nyiezi,
Akianguka, na macho yake yamefumbuka:
- 17 Namwona, wala si sasa:
Namtazama, wala si karibu:
Patatokea nyota katika Yakobo,
Itaondoka fimbo katika Israeli,
Na kupigapiga pembe za Moab,
Na kuvunjavunja waana wote wa fitina.
- 18 Na Edom itakuwa milki,
Seir tena itakuwa milki, adui zake;
Akiwa Israeli atenda kwa ujasiri.
- 19 Toka Yakobo mtawala,
Naye mharibu masalio ya mjini.
- 20 Akanwona Amalek, akatunga methali yake, akasema,
~~Mwanzo wa mataifa Amalek;~~

- Na mwisho wake kwa uharibifu. . . .
- 21 Akamwona Mkeni, akatunga methali yake, akasema,
Imara makao yako,
Na tundu lako limewekwa jabalini.
- 22 Illakini kwa kuteketea Kaini,
Hatta Asshur atakapokuchukua mfu-
ngwa.
- 23 Akatunga methali yake, akasema,
Ole wao, ataishi nani, Muungu akiyati-
mia haya ?
- 24 Lakini merikebu toka pwani kwa Kit-
tim,
Nazo zitamtesa Asshur, zitamtesa Eber,
Naye pia kwa uharibifu.
- 25 Balaam akaondoka, akaenda, akarudi ma-
hali pake : Balak naye akaenda zake.

SURA 25.

ISRAELI wakakaa Shittim, watu wakaa-
nza kufanya ukahaba na binti za Moab:
2 wakawaita watu kwa sadaka za miungu
yao ; watu wakala, wakaisujudu miungu
3 yao. Israeli akajifungia Baal-Peor : hasira
4 ya Bwana ikawaka juu ya Israeli. Bwana
akamwambia Musa, Watwae wakuu wote
wa watu, mtundikie Bwana mbele ya jua,
ipate hasira kali ya Bwana kuwaondokea
5 Israeli. Musa akawaambia waamuzi wa
Israeli, Ueni killa mmoja watu wake walio-

- 6 jifungia Baal-Peor. Hatta, tazama, mtu wa waana wa Israeli akaja, akamkaribisha kwa ndugu zake mwanamke Mmidiani machoni pa Musa, na machoni pa jamaa yote ya waana wa Israeli, waliokuwa wakilia
- 7 mlangoni pa hema ya kusanyiko. Akaona Finehas, mwana wa Eleazar, mwana wa Harun mkohani, akaondoka katika jamaa,
- 8 akatwaa mkuki mkononi: akamfuata yule mtu wa Israeli hatta katika kichumba, akawapiga wote wawili, mwanamume Mwisraeli, na mwanamke akampiga wa tumbo. Bassi teso likazuiwa kwao waana wa Israeli.
- 9 Nao waliokufa kwa teso walikuwa asharini na 'nne elfu.
- 10 Bwana akamwambia Musa, akasema,
- 11 Finehas, mwana wa Eleazar, mwana wa Harun mkohani, amenigeuzia hasira mbali kwa waana wa Israeli, kwa kuwa mwivu kwa uwivu wangu kati mwao, nisiwateke teze waana wa Israeli kwa uwivu wangu.
- 12 Kwa hiyo sema, Angalia, na upa agano langu la amani: nalo litakuwa kwake na kwa mzao wake baada yake, agano la ukohani wa milele; kwa sababu alikuwa mwivu kwa ajili ya Muungu wake, akawafanyia upatanisho waana wa Israeli. Bassi jina lake Mwisraeli aliyeuawa, aliyeuawa yeye na mwanamke Mmidiani, Timri mwana wa Salu, mkuu wa nyumba ya baba katika
- 15 Wasimeon. Na jina la mwanamke Mmidiani aliyeuawa Kozbi, binti Zur; mkuu naye wa watu wa nyumba ya baba katika Mi-

16 diani. Bwana akamwambia Musa, akisema,
 17 Wachukizeni Wamidiani, mkawapige;
 18 kwani wawachukiza ninyi kwa hila zao,
 walizowashawishia ninyi kwa jambo la
 Peor, na kwa jambo la Kozbi, binti wa
 mkuu wa Midiani, umbu lao, aliyeuawa si-
 ku ya tesu kwa jambo la Peor.

SURA 26.

IKAWA baada ya tesu, Bwana akawaa-
 mbia Musa na Eleazar mwana wa Ha-
 2 run mkohani, akisema, Fanyeni hesabu ya
 kusanyiko lote la waana wa Israeli, wenyi
 miaka asharini na zayidi, kwa nyumba za
 baba zao, wote wawezao kwenda vitani, wa
 3 Israeli. Wakasema nao Musa na Eleazar
 mkohani katika inchi sawa za Moab karibu
 4 na Yardeni kwa Yeriko, wakisema, Wenyi
 miaka asharini na zayidi; kama Bwana ali-
 vyomwamuru Musa na waana wa Israeli,
 waliotoka katika inchi ya Misri.
 5 Reuben, mzaliwa wa kwanza wa Israeli:
 waana wa Reuben: wa Hanok, jamaa ya
 Wahanok: wa Pallu jamaa ya Wapallu:
 6 wa Hezron, jamaa ya Wahezron: wa Karmi,
 7 jamaa ya Wakarmi. Hawa jamaa za Wa-
 reuben: nao waliohesabiwa wao thelatha
 8 u «robaini elfu na mia saba na thelathini.
 9 Na waana wa Pallu, Eliab. Na waana wa
 Eliab; Nemuel, na Dathan, na Abiram.
 Hawa Dathan na Abiram wale, wateule wa

- kusanyiko, walioshindana na Musa na Harun katika makutano ya Kora, waliposhindana na Bwana: ikafumbua dunia kinwa chake, ikawameza pamoja na Kora, walipokufa makutano yale; wakati moto ulipotekeza watu miteen na hamsini, wakawa ishara. Illakini waana wa Kora hawakufa.
- 12 Waana wa Simeon kwa jamaa zao: wa Nemuel, jamaa ya Wanemuel: wa Yamin, jamaa ya Wayamin: wa Yakin, jamaa wa
- 13 Wayakin: wa Zera, jamaa ya Wazera: wa
- 14 Shaul, jamaa ya Washaul. Hawa jamaa za Wasimeon, theneen u asharini elfu na miteen.
15. Waana wa Gad kwa jamaa zao: wa Zefon, jamaa ya Wazefon: wa Haggi, jamaa ya Wahaggi: wa Shuni, jamaa ya Wshuni:
- 16 ni: wa Ozni, jamaa ya Wozni: wa Eri,
- 17 jamaa ya Waeri: wa Arod, jamaa ya Waa-
- 18 rod: wa Areli, jamaa ya Waareli. Hawa jamaa za waana wa Gad kwa kuhesabiwa kwao, arobaini elfu na mia tano.
- 19 Waana wa Yuda, Er na Onan: wakafa Er na Onan katika inchi ya Kanaan.
- 20 Wakawa waana wa Yuda kwa jamaa zao; wa Shela, jamaa ya Washelani; wa Perez, jamaa ya Waperez: wa Zera, jamaa wa
- 21 zera. Wakawa waana wa Perez; wa Hezron, jamaa ya Wahezron: wa Hamul, jamaa ya Wahamul. Hawa jamaa za Yuda kwa kuhesabiwa kwao, sabwini na sita elfu na mia tano.

- 23 Waana wa Issákar kwa jamaa zao : *wa*
Tola, jamaa ya Watola : *wa* Puva, jamaa
24 ya Wapuni ; *wa* Yashub, jamaa ya Waya-
shub : *wa* Shimron, jamaa ya Washimron.
25 Hawa jamaa ya Issakar kwa kuhesabiwa
kwao, aroba u settini elfu na mia tatu.
26 Waana wa Zabulon kwa jamaa zao : *wa*
Sered, jamaa ya Wasered ; *wa* Elon jamaa
ya Waelon : *wa* Yahleel jamaa ya Wa-
27 yahleel. Hawa jamaa ya Wazabulon kwa
kuhesabiwa kwao, settini elfu na mia tano.
28 Waana wa Yusuf kwa jamaa zao : Mana-
29 sse na Efraim. Waana wa Manasse : *wa*
Makir, jamaa ya Wamakir : na Makir
akamzaa Gilead : *wa* Gilead, jamaa ya Wa-
30 gilead. Hawa waana wa Gilead : *wa* Iezer,
jamaa ya Waiezer : *wa* Helek, jamaa ya
31 Wahelek ; na *wa* Asriel, jamaa ya Waasriel :
na *wa* Shechem, jamaa ya Washechem :
32 na *wa* Shemida, jamaa ya Washemida : na
33 *wa* Hefer jamaa ya Wahefer. Na Zelofehad
mwana wa Hefer hakuwa na waana, illa
binti : na majina ya binti za Zelofehad
Mahlá, na Noa, Hogla, Milka, na Tirza.
34 Hawa jamaa za Manasse : nao waliohesabi-
wa wao theneen u hamsini elfu na mia saba.
35 Hawa waana wa Efraim kwa jamaa zao :
wa Shuthela, jamaa ya Washuthela : *wa*
Beker, jamaa ya Wabeker : *wa* Tahan,
36 jamaa ya Watahan. Na hawa waana wa
37 Shuthela : *wa* Eran, jamaa ya Waeran. Ha-
wa jamaa za waana wa Efraim kwa kuhe-

sabiwa kwao, theneen u thelathini elfu na mia tano. Hawa waana wa Yusuf kwa jamaa zao.

38 Waana wa Benjamin kwa jamaa zao : wa Bela, jamaa ya Wabela : wa Ashbel, jamaa ya Waashbel : wa Ahiram, jamaa ya Waahiram :

39 wa Shefufam, jamaa ya Washufam :
40 wa Hufam, jamaa ya Wahufam. Na waana wa Bela wakawa Ard na Naaman : jamaa ya Waard : wa Naaman, jamaa ya Wanaaman.

41 Hawa waana wa Benjamin kwa jamaa zao : nao waliohesabiwa wao hamsi u arobaini elfu na sita mia.

42 Hawa waana wa Dan kwa jamaa zao : wa Shuham, jamaa ya Washuham. Hawa jamaa za Dan kwa jamaa zao. Jamaa zote
43 za Washuhan, kwa kuhesabiwa kwao, aroba u settini elfu na mia 'nne.

44 Waana wa Asher kwa jamaa zao : wa Imna, jamaa ya Waimna : wa Ishvi, jamaa ya Waishvi : wa Beria, jamaa ya Waberia.

45 Wa waana wa Beria : wa Heber, jamaa ya Waheber : wa Malkiel, jamaa ya Wamalkiel. Na jina la binti Asher Sera.

47 Hawa jamaa za waana wa Asher kwa kuhesabiwa kwao, thelatha u hamsini elfu na mia 'nne.

48 Waana wa Naftali kwa jamaa zao : wa Yahzeel, jamaa ya Wayahzeel : wa Gu i, jamaa ya Waguni : wa Yezer, jamaa ya Wayezer : wa Shillem, jamaa ya Washillem.

50 Hawa jamaa za Naftali kwa jamaa zao : nao waliohesabiwa wao hamsi u arobaini

elfu na mia 'nne.

- 51 Hawa waliohesabiwa wa waana wa Israeli, sita mia elfu na elfu moja na mia saba na thelathini.
- 52 Bwana akamwambia Musa, akisema,
53 Hawa watagawanyikiwa inchi kuwa milki
54 kwa hesabu ya majina. Wakizidi utawazidishia milki, wakipunguka utawapunguzia milki : kila mtu kwa kadiri yao waliohesabiwa kwake atapewa milki. Illakini kwa
55 kura itagawanyika inchi : kwa majina ya
56 makabila ya baba zao wataimiliki. Kwa kura milki itagawanyika kwao walio wengi na kwao walio haba.
- 57 Na hawa waliohesabiwa wa Walawi kwa jamaa zao : wa Gershon, jamaa ya Wager-shon : wa Kohath, jamaa ya Wakohath :
58 wa Merari, jamaa ya Wamerari. Hawa jamaa za Lawi : jamaa ya Walibui, jamaa ya Wahebron, jamaa ya Wamahli, jamaa ya Wamushi, jamaa ya Wakora. Kohath
59 akamzaa Amram. Na jina la mkewe Amram Yokebed biati Lawi, aliyemzaa Lawi katika Misri : akamzalia Amram Harun na
60 Musa, na Maryamu umbu wao. Harun akawzaa Nauab na Abihu, Eleazar na
61 Itamar. Wakafa Nadab na Abihu, wali-
62 potoa moto mgeni mbele ya Bwana. Nao waliohesabiwa wao thelatha u asharini elfu, kila mume mwenyi mwezi na zayidi : kwani hawakuhesabiwa kati ya waana wa Israeli, kwa sababu hawakupewa maki kati ya waana wa Israeli.

- 63 Hawa waliohesabiwa na Musa na Eleazar
mkohani; waliowahasibu waana wa Israeli
katika inchi sawa ya Moab karibu na Yar-
64 deni kwa Yeriko. Lakini katika hawa
hapakuwa mtu wao, waliohesabiwa na
Musa na Harun mkohani; waliowahasibu
65 waana wa Israeli kwa bara ya Sinai. Kwa-
ni Bwana amewasemea, Kufa watakufa
katika bara. Wala hakuwalia mtu katika
wao, illa Kaleb mwana wa Yefunne, na Isa
mwana wa Nun.

SURA 27.

- N** DIPO wakakaribia binti za Zelofehad,
mwana wa Hefer, mwana wa Gilead,
mwana wa Makir, mwana wa Manasse,
wa jamaa za Manasse mwana wa Yusuf:
na naya majina ya binti zake; Mahla, Noa,
2 na Hogla, na Milka, na Tirza. Wakasima-
ma mbele ya Musa, na mbele ya Eleazar
mkohani, na mbele ya wakuu na jamaa yote,
mlangoni pa hema ya kusanyiko, wakisema,
3 Baba yetu alikufa nyikani, wala hakuwa-
mo kati ya jamaa yao waliokusanyika juu
ya Bwana katika jamaa ya Kora: lakiui
thambi yake aliyoitia; wala hakuwa na wa-
4 ana. Mbona jina la baba yetu liondolewe
katika kati ya jamaa yake, kwa sababu
hakuwa na mwana? Utupe naswi mali ka-
5 ti ya ndugu za baba wetu. Musa akamle-
6 tea Bwana hukumu yao. Bwana akamwa-
7 mbia Musa akisema, Wasemavyo binti za

Zelofehad ndivyo : kupewa watapewa mali ya milki kati ya ndugu za baba yao ; nawe
 8 utawafikilizia milki ya baba yao. Na waana wa Israeli utawaambia, ukisema, Akifa mtu hana mwana, bassi mtamfikilizia binti
 9 yake milkiye. Na kama hana binti, bassi
 10 mtawapa nduguze milki yake. Na kama hana ndugu, bassi ndipo utawapa ndugu za
 11 baba e milki yake. Na kama babaye hana ndugu, bassi mtampa milkiye aliye karibu kwake wa jamaa yake, naye ataipata : na itakuwa kwa waana wa Israeli kwa sheria ya hukumu, kama Bwana alivyomwamuru
 12 Musa. Bwana akamwambia Musa, Panda kwa mlima huu wa Abarim, ukaione inchi
 13 niliyowapa waana wa Israeli. Na ukiisha kuiona ut kusanyika nawe kwa watu wako, kama Harun nduguyo alivyokusanyika:
 14 kwa sababu mmeasi juu ya neno langu barani mwa Zin, kwa makasirisho ya kusanyiko, kunitakasa machoni pao, penyi maji. (Maji ya Meriba haya kwa Kadesh. katika
 15 bara ya Zin.) Musa akamwambia Bwana,
 16 akisema, Aagize Bwana, Muungu wa roho
 17 za mili yote, mtu juu ya kusanyiko, atakayetoka mbele yao, na kuingia mbele yao, atakayewatoa na kuwaingiza ; wasiwe kusanyiko la Bwana kama kondoo wasio na
 18 mohungaji. Bwana akamwambia Musa, Ujitwalie Isa mwana wa Nun, mtu mwenyi Roho, ukatie mkono wako juu yake ;
 19 ukamweke mbele ya Eleazar mkohani, na mbele ya kusanyiko lote ; akaamriwe ma-

- 20 choni pao. Nawe utamtilia ya heshima yako, kusanyiko lote la waana wa Israeli
- 21 wapate kusikiliza. Na mbele ya Eleazar mkohani atasimama, atakayemwulizia kwa hukumu ya Urimi mbele ya Bwana: kwa neno lake watatoka, na kwa neno lake wataingia, yeye na waana wa Israeli wote
- 22 naye, hatta kusanyiko lote. Akafanya Musa kama Bwana alivyomwamuru: akamtwaa Isa wa Nun, akamweka mbele ya Eleazar mkohani, na mbele ya kusanyiko
- 23 lote: akamtia mikono, naye akaamriwa kama Bwana alivyosema kwa mkono wa Musa.

SURA 28.

- B**WANA akanwambia Musa, akisema,
 (2) Uwaamrie waana wa Israeli, ukawaambie, Sadaka yangu, mikate yangu ya matoleo yangu ya moto, ya nukato la utulizo kwangu, mtaangalia kunitolea kwa
- 3 wakati wake. Nawe utawaambia, Hiyo ya moto mtakayomtolea Bwana; waana kondoo waume wa mwaka wa kwanza, wakamilifu, wawili kwa siku, kwa kafara ya
- 4 dayima. Mwana kondoo mmoja mtamtoa assubuhi, na mwana kondoo wa pili mtamtoa
- 5 kati ya jioni mbili; na ya kumi ya efa moja ya unga mzuri kwa sadaka ya unga, imechanganyika nayo ya 'nne ya hini ya mafuta
- 6 ta yaliyopigwa. Kafara ya dayima, iliyo-

- amriwa kwa mlima Sinai kuwa nukato la utulizo, sadaka ya moto kwa Bwana.
- 7 Na miminiko lake ya 'une ya hini kwa mwana kondoo mmoja: panapo patak tifu utammiminia Bwana miminiko la kileo.
- 8 Na mwana kondoo wa pili utamtoa kati ya jioni mbili: kama sadaka ya unga ya assubuhi, na kama miminiko lake, ndivyo utakavyoitoa, sadaka kwa moto, ya nukato la utulizo kwa Bwana.
- 9 Na siku ya sabato waana kondoo waume wawili wa mwaka wa kwanza wakamilifu, na sehemu za kumi mbili za unga mzuri, kwa sadaka ya unga, uliochanganyika na
- 10 mafuta, na miminiko lake: kafara hii ya sabato kwa sabato, juu ya kafara ya dayima na miminiko lake.
- 11 Na kwa mianzo ya miezi yenu mtamtolea Bwana kafara; ndama wawili, na kondoo mume mmoja, waana kondoo waume saba wa mwaka wa kwanza wakamilifu;
- 12 Na sehemu za kumi tatu za unga mzuri kwa sadaka ya unga, uliochanganyika na mafuta kwa killa ng'ombe, na sehemu za kumi mbili za unga mzuri kwa sadaka ya unga, umechanganyika na mafuta, kwa
- 13 kondoo mume mmoja; na sehemu ya kumi ngingine ya unga mzuri uliochanganyika, na mafuta kwa sadaka ya unga kwa killa mwana kondoo; kafara ya nukato la utulizo,
- 14 sadaka kwa moto kwa Bwana. Na mamiminiko yao yatakuwa nussu ya hini ya mvinyo kwa ng'ombe, na theluth ya

- hini kwa kondoo mume, na robo ya hini kwa mwana kondoo: hiyo kafara ya mwezi kwa mwezi, miezi yote ya mwaka.
- 15 Na mbuzi mume mmoja sadaka ya thambi kwa Bwana; itatolewa juu ya kafara ya dayima na miminiko lake.
- 16 Na mwezi wa kwanza, siku ya arobata-
- 17 shara ya mwezi, pasaka ya Bwana. Na siku ya hamstashara ya mwezi huu siku kuu: siku saba visivyochachwa vitaliwa.
- 18 Siku ya kwanza wito mtakatifu; hamtatumika kazi yo yote: lakini mtatoa sadaka
- 19 kwa moto, kafara kwa Bwana; ndama wawili, na kondoo mume mmoja, na waana kondoo waume saba wa mwaka wa kwanza: wakamilifu watakuwa kwenu: na sadaka yao ya unga, unga mzuri uliochanganyika na mafuta: sehemu za kumi tatu mtatoa kwa ng'ombe, na sehemu za kumi
- 21 mbili kwa yule kondoo mume; sehemu ya kumi nyingine utatoa kwa kila mwana kondoo wa wale saba; mbuzi mume mmoja kwayo ya thambi, kujifanyia upatanisho.
- 22 Juu ya kafara ya assubuhi, iliyo kwa kafara ya dayima mtatoa hizi. Kwa namna hii mtatoa siku kwa siku, siku saba, mkate wa sadaka kwa moto, wa nukato la utulizo kwa Bwana: kutolewa juu ya kafara ya
- 25 dayima, na miminiko lake. Na siku ya saba utakuwa wito mtakatifu kwenu; hamtatumika kazi yo yote.
- 26 Tena siku ya malimbuko mtakapomtolea Bwana sadaka mpya ya unga katika juu

zenu, utakuwa wito mtakatifu kwenu;
 27 hamtatumika kazi yo yote : lakini mtamto-
 lea Bwana kafara kwa nukato la utulizo ;
 ndama wawili, kondoo mume mmoja, waa-
 na kondoo saba waume wa mwaka wa
 28 kwanza ; na sadaka yao ya unga, unga
 mzuri uliochanganyika na mafuta, sehemu
 za kumi tatu kwa killa ng'ombe, sehemu
 za kumi mbili kwa yule kondoo mmoja,
 29 na sehemu ya kumi ngingine kwa killa mwa-
 30 na kondoo wa wale saba ; mbuzi mume
 31 mmoja, mjifanyizie upatanisho. Juu ya
 kafara ya dayima, na sadaka yake ya unga,
 mtazitoa (kamilifu zitakuwa kwenu,) na
 mamiminiko yao.

SURA 29.

NA mwezi wa saba, ya kwanza ya mwe-
 zi, utakuwa wito mtakatifu kwenu ;
 hamtatumika kazi yo yote : ni siku ya ku-
 2 pigia paanda kwenu. Nanyi mtatoa kafa-
 ra kwa nukato la utulizo kwa Bwana ;
 ndama mmoja, kondoo mume mmoja, waa-
 na kondoo waume saba wa mwaka wa
 3 kwanza wakamilifu : na sadaka yake ya
 unga, unga mzuri uliochanganyika na
 mafuta, sehemu za kumi tatu kwa ng'ombe,
 sehemu za kumi mbili kwa kondoo mume,
 4 na sehemu ya kumi moja kwa killa mwana
 5 kondoo wa wale saba : na mbuzi mume
 mmoja kwayo ya thambi, mjifanyizie upa-
 6 tanisho : juu ya kafara ya mwezi mpya, na

- sadaka yake ya unga, na kafara ya dayi-
 ma, na sadaka yake ya unga, na mamimini-
 ko yake, kwa sheria yake, kuwa nukato la
 utulizo, matoleo kwa moto kwa Bwana.
- 7 Na ya kumi ya mwezi huu wa saba utaku-
 wa wito mtakatifu kwenu; nanyi mtatesa
 nafsi zenu; hamtatumika kazi yo yote:
- 8 lakini mtamtolea Bwana kafara kwa nukato
 la utulizo; ndama mmoja, kondoo mume
 mmoja, waana kondoo waume saba wa
 mwaka wa kwanza; wakamilifu watakuwa
- 9 kwenu; na sadaka yake ya unga, unga
 mzuri uliochanganyika na mafuta, sehemu
 za kumi tatu kwa yule ng'ombe, sehemu
 za kumi mbili kwa yule kondoo mume,
- 10 sehemu ya kumi ngingine kwa killa mwana
- 11 kondoo wa wale saba: mbuzi mume mmoja
 kwayo ya thambi; juu yake ya thambi
 ya upatanisho, na kafara ya dayima, na
 sadaka yake ya unga, na mamiminiko
 yake.
- 12 Na siku ya hamstashara ya mwezi wa
 saba utakuwa wito mtakatifu kwenu; ha-
 mtatumika kazi yo yote, nanyi mtamfanyia
- 13 Bwana siku kuu siku saba: nanyi mtamtolea
 kafara, sadaka kwa moto, ya nukato la
 utulizo kwa Bwana; ndama thelitashara,
 kondoo waume wawili, waana kondoo wa-
 ume arobatashara wa mwaka wa kwanza;
- 14 wakamilifu watakuwa: na sadaka yake ya
 unga, unga mzuri uliochanganyika na
 mafuta, sehemu za kumi tatu za killa
 ng'ombe wa wale thelitashara, sehemu za

- kumi mbili za killa kondoo mume wa wale
 15 wawili, na sehemu ya kumi ngingine ya killa
 16 mwana kondoo wa wale arobatashara: na
 mbuzi mume mmoja kwayo ya thambi;
 juu ya kafara ya dayima, sadaka yake ya
 unga, na miminiko lake.
- 17 Na siku ya pili ndama thenashara, ko-
 ndoo waume wawili, waana kondoo waume
 arobatashara wa mwaka wa kwanza wa-
 18 kamilifu; na sadaka yake ya unga na
 mamiminiko yake kwa ng'ombe, na kwa
 kondoo waume, na kwa wanaa kondoo,
 19 kwa hesabu yao, ilivyoagizwa: na mbuzi
 mume mmoja kwayo ya thambi; juu ya
 kafara ya dayima, na sadaka yake ya unga,
 na mamiminiko yake.
- 20 Na siku ya tatu ng'ombe edashara, ko-
 ndoo waume wawili, waana kondoo waume
 arobatashara wa mwaka wa kwanza waka-
 21 milifu; na sadaka yake ya unga, na mami-
 miniko yake kwa ng'ombe, na kwa kondoo
 waume, na kwa waana kondoo, kwa hesa-
 22 bu yao, ilivyoagizwa: na mbuzi mume
 mmoja kwayo ya thambi; juu ya kafara ya
 dayima, na sadaka yake ya unga, na
 miminiko lake.
- 23 Na siku ya 'nne ng'ombe kumi, kondoo
 waume wawili; waana kondoo waume aro-
 batashara wa mwaka wa kwanza wakami-
 24 lifu: sadaka yake ya unga, na mamiminiko
 yake, kwa ng'ombe, na kwa kondoo wau-
 me, na kwa waana kondoo, kwa hesabu
 yao, ilivyoagizwa; na mbuzi mume mmoja

kwayo ya thambi; juu ya kafara ya dayima, sadaka yake ya unga, na miminiko lake.

- 26 Na siku ya tano ng'ombe kenda, kondoo waume wawili, waana kondoo waume aro-
- 27 batashara wa mwaka wa kwanza wakamili-
lifu: na sadaka yake ya unga, na mamimi-
niko yake kwa ng'ombe, kwa kondoo wau-
me, na kwa waana kondoo, kwa hesabu yao,
- 28 ilivyoagizwa: na mbuzi mume mmoja
kwayo ya thambi; juu ya kafara ya dayi-
ma, na sadaka yake ya unga, na miminiko
lake.
- 29 Na siku ya sita ng'ombe wanane, kondoo
waume wawili, waana kondoo waume aro-
batashara wa mwaka wa kwanza waka-
30 milifu: na sadaka yake ya unga na mami-
miniko yake kwa ng'ombe, na kwa kondoo
waume, na kwa waana kondoo, kwa hesa-
31 bu yao, ilivyoagizwa: na mbuzi mume
mmoja kwayo ya thambi; juu ya kafara
ya dayima, sadaka yake ya unga, na mi-
miniko lake.
- 32 Na siku ya saba ng'ombe saba, kondoo
waume wawili, waana kondoo waume aro-
batashara wa mwaka wa kwanza wakami-
33 lifu, na sadaka yake ya unga, na mamimi-
niko yake kwa ng'ombe, kwa kondoo wau-
me, na kwa waana kondoo, kwa hesabu
34 yao, ilivyoagizwa: na mbuzi mume mmoja
kwayo ya thambi; juu ya kafara ya dayi-
ma, sadaka yake ya unga, na miminiko
lake.
- 35 Siku ya nane yatakuwa makutano makuu

- 36 kwenu : hamtatumika kazi yo yote : lakini mtamtolea Bwana kafara, matoleo kwa moto, ya nukato la utulizo : ng'ombe mmoja, kondoo mume mmoja, waana kondoo waume saba wa mwaka wa kwanza waka-
- 37 milifu : sadaka yake ya unga na mamiminiko yake kwa ng'ombe, kwa kondoo mume, na kwa waana kondoo, kwa hesabu yao,
- 38 ilivyoagizwa : na mbuzi mume mmoja kwayo ya thambi ; juu ya kafara ya siku zote, na sadaka yake ya unga, na miminiko lake.
- 39 Hizi mtakazomtolea Bwana kwa siku kuu zenu, juu ya nathiri zenu, na juu ya sadaka zenti za moyo, kuwa kafara zenu, na kuwa sadaka zenu za unga, na kuwa mamiminiko yenu, na kuwa thabihu zenu za
- 40 amani. Musa akawaambia waana wa Israeli kwa yote Bwana aliyomwamuru Musa.

SURA 30.

MUSA akawaambia wakuu wa makabila ya waana wa Israeli akisema, Hi-

2 li ndilo Bwana aliloamuru. Mtu amwekeapo Bwana nathiri, ao kuapa kiapo cha kujifungia roho mafungo, neno lake hatalitia unajisi ; atatenda kwa yote yatokayo ka-

3 nwani kwake. Tena mwanamke amwekeapo Bwana nathiri, na kujifungia mafungo nyumbani mwa baba katika ujana wake ;

4 akisikia babaye nathiri yake, na mafungo aliyojifungia roho, naye baba akiwua

- kimya: bassi nathiri zake zote zitakaa, na killa fungo alilojifungia roho litakaa.
- 5 Lakini baba akimkataza siku asikiapo, killa nathiri yake, na killa fungo alilojifungia roho, hazitakaa: naye Bwana atamwachilia, kwa sababu babaye amemkataza.
- 6 Naye akiwa na mume, na nathiri zake juu yake, ao midomo yake kuharakisha
- 7 neno, alilojifungia roho; akisikia mumeye, naye akimwia kimya siku asikiapo: bassi nathiri zake zitakaa, na mafungo yake
- 8 aliojifungia roho yatakaa. Lakini mume akimkataza siku asikiapo; bassi atatangua nathiri yake iliyo juu yake, na neno liloharakisha midomo, alilojifungia roho: na
- 9 Bwana atamwachilia. Lakini nathiri yake mjaani, ao yake aliyefukuzwa, killa neno
- 10 alilojifungia roho, litakaa juu yake. Na kama ameweka nathiri nyumbani mwa mumeye, ao kujifungia roho mafungo
- 11 kwa kiapo, naye mume amelisikia, na kumwia kimya, asimkataze; bassi nathiri zake zote zitakaa, na killa fungo alilojifungia roho litakaa. Lakini kama kutangua amezitangua mumeye siku alipozisikia; bassi halitakaa lo lote lililotoka midomoni mwake la nathiri zake, ao la fungo la roho yake: mumeye amezitangua; naye
- 13 Bwana atamwachilia. Killa nathiri, na killa kiapo kimpungiacho roho kwa kuitesa, ya mumeye kuliyakinisha, ao ya mume
- 14 meye kulitangua. Lakini kama mumeye siku kwa siku humwia kimya tu; bass

humyakinishia nathiri zake zote, ao mafungo yake yote yaliyo juu yake: ameyakinisha, kwa sababu alimwia kimya siku aliposikia. Lakini kutangua akiyatangua 15 asikiapo; bassi atamchukulia uovu. Hizi 16 sheria, Bwana alizomwamuru Musa, kati ya mtu na mke wake, kati ya baba na binti yake, katika ujana wake, nyumbani mwa babaye.

SURA 31.

BWANA akamwambia Musa, akisema, (2) Uwalipize kisasi waana wa Israeli juu ya Wamidian: baadaye utakusanyika 3 kwa watu wako. Musa akawaambia watu, akisema, Wapangeni watu katika miongoni mwenu kwa vita, wapate kwenda juu ya Midian, kumfanyizia Bwana kisasi juu 4 ya Midian. Kwa killa kabila watu elfu, katika makabila yote ya Israeli, mtawapeleka 5 vitani. Bassi wakatolewa katika elfu za Israeli, wa killa kabila elfu, elfu thenasha- 6 ra wenyi selaha za vita. Musa akawapeleka, elfu kwa kabila, vitani, wao na Finahas mwana wa Eleazar mkohani, vitani, pamoja na vyombo vya patakatifu na mapanda ya kupigia mbiu mkononi. 7 Wakapigana juu ya Midian, kama Bwana alivyomwamuru Musa; wakamwua killa 8 mwanamume. Wakawaua wafalme wa Midian, pamoja na wangine waliouawa; Evi, na Rekem, na Zur, na Hur, na Reba,

- wafalme watano wa Midian : Balaam naye mwana wa Beor wakamwua kwa upanga.
- 9 Waana wa Israeli wakachukua wafungwa waanawake wa Midian na wadogo wao : na ng'ombe zao zote, na kondoo zao zote,
- 10 na mali zao zote, wakatwaa mateka. Na miji yao yote makaoni mwao, na matuo
- 11 yao yote wakateketeza kwa moto. Wakachukua mapato yote, na mateka yote,
- 12 ya watu na ya nyama. Na wafungwa, na mateka, na mapato wakawaletea Musa na Eleazar mkohani, na kusanyiko lote matuoni kwa inchi sawa ya Moab karibu na Yardeni kwa Yeriko.
- 13 Na Musa, na Eleazar mkohani, na wakuu wote wa kusanyiko wakatoka kuwalaki
- 14 nje ya matuo. Akakasirika Musa na maakida wa jeshi, wakuu wa elfu na wakuu wa mia, waliokuja katika serikari ya
- 15 vita. Musa akawaambia, Mmewaacha
- 16 hayi waanawake wote? Angalieni, hawa ndio waliowaletea, kwa shauri lake Balaam, waana wa Israeli kosa juu ya Bwana kwa
- 17 neno la Peor, likawa teso kati ya kusanyiko la Bwana. Bassi sasa mwueni killa mume wa wale wachanga, na killa mwana-
- 18 mke aliyemjua mtu kwa kulala na mume mwueni. Lakini watoto waanawake wote wasiomjua mtu kwa kulala na mume mji-
- 19 hifathieni hayi. Nanyi tuceni nje ya matuo siku saba : killa aliyewa mtu, na killa aliyegusa waliouawa, mjitakase siku ya tatu, na siku ya saba, ninyi na wafungwa

- 20 wenu. Na kwa killa vazi, navyo vyote vilivyo vya ngozi, na kwa killa cha nyele za mbuzi, navyo vyote vilivyo vya mti, mtajitakasa. Eleazar mkohani akawaambia watu wa vita waliokwenda kupigana, Hii sheria ya torati Bwana aliyomwamuru Musa; Illakini thahabu na fetha, shaba, chuma, bati, na risasi, neno lo lote liwezalo kuingia motoni, mtapitisha motoni, nayo itakuwa safi; illa kwa maji ya kujitenga itatakasika: na yote yasiyoingia motoni mtapitisha majini. Nanyi mtafua nguo zenu siku ya saba, nanyi mtakuwa safi, hatta baadaye mtaingia matuoni.
- 25 Bwana akamwambia Musa akisema,
26 Fanya hesabu ya mateka ya wafungwa, na wa watu na wa nyama, wewe na Eleazar mkohani, na wakuu wa baba za kusanyiko: ukayagawanye mateka sehemu mbili; kati ya watu mashujaa wa vita waliokwenda kupigana, na kusanyiko lote: ukawatoze watu wa vita waliokwenda kupigana kodi ya Bwana: mmoja katika mia tano, wa watu na wa ng'ombe, na wa makundi: katika ile nussu iliyo yao twaa, ukampe Eleazar mkohani, ya kuinuliwa ya Bwana. Na katika ile nussu ya waana wa Israeli utamtwaa mmoja aliyeshikwa wa killa hamsini, wa watu, wa ng'ombe, wa punda na wa makundi, wa nyama zote, nawe utawapa Walawi, walindao malinzi ya masikani ya Bwana. Wakafanya Musa na Eleazar mkohani kama Bwana alivyomwamuru

- 32 Musa. Nayo yaliyotwaliwa, mabaki ya mateka waliyoyatwaa watu wa vita, yaka-wa kondoo sita mia sabwini na tano
- 33 elfu, na ng'ombe sabwini na mbili elfu,
- 34 na punda settini na moja elfu, (35) na watu thelathini na mbili elfu jumla, wa waana-wake wasiomjua mtu kwa kulala na mume.
- 36 Na ile nussu, sehemu yao waliokwenda kupigana, ikawa hesabu yake kondoo mia
- 37 tatu thelathini na saba elfu na mia tano: na kodi yake Bwana ya kondoo ikawa sita
- 38 mia na sabwini na watano. Nazo ng'ombe thelathini na sita elfu; wa hizo kodi yake
- 39 Bwana sabwini na wawili. Nazo punda thelathini elfu na mia tano; wa hizo
- 40 kodi yake Bwana, settini na mmoja. Nao watu sitashara elfu; wa hao kodi yake
- 41 Bwana watu thelathini na wawili. Nayo kodi, ya kuinuliwa yake Bwana, Musa akampa Eleazar mkohani, kama Bwana
- 42 alivyomwamuru Musa. Na katika ile nussu ya waana wa Israeli, Musa aliyowa-
- 43 katia watu waliopigana, (ikawa nussu yao kusanyiko kondoo mia tatu thelathini na
- 44 saba elfu na mia tano, na ng'ombe thelathini
- 45 na sita elfu, na punda thelathini elfu na
- 46 mia tano, na watu sitashara elfu;)
- 47 hatta katika nussu yao waana wa Israeli, Musa akatwaa mmoja aliyeshikwa wa
- 48 killa hamsini, wa watu na wa nyama, akawapa Walawi waliolinda malinzi ya masikani ya Bwana; kama Bwana alivyo-
- mwamuru Musa. Wakamkaribia Musa

- waliowasimamia elfu za jeshi, wakuu wa
 49 elfu, na wakuu wa mia: wakamwambia Musa, Watumwa wako wamefanya hesabu ya watu wa vita wa mikononi mwetu, wala hakupunguka mtu
 50 mmoja wetu. Naswi tumemletea Bwana matoleo, killa mtu aliyoyapata, ya johari za thahabu, mitali, na timbi, pete za muhuri, vipini na vikuku, kujifanyia upatanisho wa roho zetu mbele ya Bwana.
 51 Wakaipokea thahabu kwao Musa na Eleazar mkohani, zote johari zilizofanyiziwa.
 52 Ikawa thahabu yote ya sadaka ya kuinuliwa waliomwinulia Bwana, ya wakuu wa elfu, na ya wakuu wa mia, shekeli sitashara
 53 elfu saba mia na hamsini. (Nao watu wa vita wamejitwalia killa mtu mateka
 54 yake.) Wakaipokea thahabu Musa na Eleazar mkohani kwao wakuu wa elfu na wa mia wakaileta hemani mwa kusanyiko, ukumbusho wa waana wa Israeli mbele ya Bwana.

SURA 32.

BASSI waana wa Reuben na waana wa Gad walikuwa na ng'ombe wengi sana : na walipoiona inchi ya Yazer, na inchi ya Gilead, ya kuwa mahali, tazama, mahali pa ng'ombe ; waana wa Gad na waana wa Reuben wakaja wakasema na Musa na Eleazar mkohani, na wakuu wa kusanyiko,
 2
 3 wakisema, Ataroth, na Dibon, na Yazer,

na Nimra, na Heshbon, na Eleale, na Se-
 4 bam, na Nebo, na Beon, inchi aliyoipiga
 Bwana mbele ya kusanyiko la Israeli,
 inchi ya ng'ombe, nasi watumwa wako
 5 tunao ng'ombe. Wakasema, Kama tume-
 ona kibali machoni pako, tupewe inchi
 hii watumwa wako tuimiliki; usituvushe
 6 Yardeni. Musa akawaambia waana wa
 Gad, na waana wa Reuben, Ndugu zenu
 waende vitani, nanyi kukaa kitako hapa?
 7 Na mbona mwawavunjia mioyo waana wa
 Israeli wasivuke hatta inchi Bwana aliyo-
 8 wapa? Ndivyo walivyotenda baba zenu,
 nilipowapeleka katika Kadesh-barnea kui-
 9 tazama inchi. Kwani walipopanda boonde-
 ni kwa Eshkol, na kuitazama inchi, wali-
 wavunjia waana wa Israeli mioyo, wasiingie
 10 inchi Bwana aliyowapa. Ikawaka hasira
 yake Bwana siku ile, akaapa, akisema,
 11 Hakika hapana mtu wao waliopanda kuto-
 ka Misri, wenyi miaka asharini na zayidi,
 atakayeiona inchi niliyomwapia Ibrahimu,
 na Isaak, na Yakob; kwa sababu hawa-
 12 kunifuata halisi, illa Kaleb mwana wa
 Yennunne Mkenizzi, na Isa mwana wa
 Nun: kwa sababu wamemfuata Bwana ha-
 13 lisi. Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Isra-
 eli, akawasafirisha barani huko na huko mi-
 aka arobaini, hatta walipoangamia, waliofa-
 nya maovu machoni pa Bwana, kizazi cho-
 14 te. Nanyi, angalieni, mmeondoka mahali
 pa baba zenu, uzidio wa watu wenyi tha-
 mbi, kuongeza zayidi hasira kali ya Bwana

- 15 kwa Israeli. Kwani mkigeuka katika nyuma yake, atawaacha naye tena barani ;
- 16 nanyi mtawaharibu watu hawa wote. Wakankaribia, wakasema, Tutawajengea hapu ng'ombe zetu mazizi, na wadogo wetu
- 17 miji : naswi wenyewe tutakuwa tayari na selaha zetu kwenda mbele ya waana wa Israeli, hatta tutakapowapeleka kwao ; na wadogo wetu watakaa katika miji yenyi boma kwa sababu yao wakaao inchi.
- 18 Hatutarudi nyumbani mwetu, hatta waana wa Israeli watakapokuwa wanamiliki killa
- 19 mtu milki yake. Kwani hatutamiliki pamoja nao ng'ambo ile ya Yardeni na mbele ; kwa sababu milki yetu imetuangukia ng'ambo hii ya Yardeni kwa mashariki.
- 20 Akawaambia Musa, Kama mtayafanya haya ; kama mtavaa selaha mwende mbele ya
- 21 Bwana vitani, na killa mtu wenu mwenyi selaha atavuka Yardeni mbele ya Bwana, hatta atakapokwisha kufukuza adui zake
- 22 mbele yake, nayo inchi kushindwa mbele ya Bwana : ndipo mtarudi, msiwe na hatiya kwa Bwana, wala kwa Israeli ; na kwenu inchi hii itakuwa kwa mali mbele
- 23 ya Bwana. Lakini msipofanya haya, angalieni, mtakuwa mmekosa juu ya Bwana : mkajue, thambi yenu itakayowapatiliza.
- 24 Wajengeeni wadogo wenu miji, na kondoo zenu mazizi ; mtafanya yale yaliyotoka kanwani mwenu. Wakasema na
- 25 Musa waana wa Gad na waana wa Reuben, wakisema, Watunwa wako watafanya ka-

- 26 ma bwanangu aamuravyo. Wadogo wetu, wake wetu, makundi yetu, na ng'ombe zetu zote watakuwako mijini mwa Gilead :
- 27 lakini watumwa wako watavuka, killa mtu aliye na selaha zake apigane, mbele ya Bwana vitani, kama bwanangu asemavyo.
- 28 Bassi Musa akawaagiza Eleazar mkohani, na Isa mwana wa Nun, na wakuu wa baba za makabila ya waana wa Israeli.
- 29 Musa akawaambia, Kama waana wa Gad na waana wa Renben watavuka Yardeni nanyi, killa mtu aliye na selaha kwa vita, mbele ya Bwana, nayo inchi itashindwa mbele yenu; ndipo mtawapa inchi ya
- 30 Gilead kuwa mali; lakini wasipovuka nanyi wenyi selaha, watapokea kati mwenu
- 31 katika inchi ya Kanaan. Wakajibu waana wa Gad, na waana wa Reuben wakisema, Kama Bwana alivyowaambia watu-
- 32 mwa wako, ndivyo tutakavyofanya. Tutavuka wenyi selaha mbele ya Bwana inchini mwa Kanaan, na mali ya milki yetu kwetu ng'ambo ya Yardeni. Musa akawapa waana wa Gad, na waana wa Reuben, na nusu kabila ya Manasse mwana wa Yusuf, ufalme wa Sidon, mfalme wa Waamori, na ufalme wa Og mfalme wa Bashan, inchi kwa miji yake yenyi mipaka, miji ya inchi iliyozunguka.
- 34 Wakajenga waana wa Gad Dibon, na Ataroth, na Aroer; na Ataroth-Shofan, na
- 35 Yazer, na Yog-beha; na Bet-nimra, na
- 36 Bet-haran : miji yenyi boma na mazizi ya

37 kondoo. Waana wa Reuben wakajenga
 38 Heshbon, na Eleale, na Kiriathaim; na
 Nebo, na Baal-meon, (ikibadilika majina,) na Sibma : wakaiita kwa majina *mangine*,
 39 miji waliyoijenga, Na waana wa Makir mwana wa Manasse wakaenda Gilead, wakaitwaa, wakawanyang'anya Waamori
 40 wa humo. Musa akampa Makir mwana
 41 wa Manasse Gilead, akakaa humo. Akae-nda Yair mwana wa Manasse akaitwaa
 42 miji yake, akaiita Havvoth-Yair. Akae-nda Noba akatwaa Kenath, na vijiji vyake, akaiita Noba kwa jina lake.

SURA 33.

HIZI safari za waana wa Israeli, walipotoka inchi ya Misri kwa majeshi yao chini ya mkono wa Musa na Harun.
 2 Musa akaandika walivyotoka kwa safari zao kwa amri za Bwana : na hizi safari zao
 3 walivyotoka. Wakasafiri kutoka Ramese mwezi wa kwanza, siku ya hamstashara ya mwezi wa kwanza ; siku ya pili yake Pasaka waana wa Israeli wakatoka kwa mkono wa juu machoni pa Wamisri wote,
 4 walipokuwa Wamisri wakizika wazaliwa wa kwanza wao wote, Bwana aliowapiga kati mwao : juu ya miungu yao tena Bwana akafanya hukumu. Waana wa Israeli wakasafiri kutoka Ramese, wakatua
 6 Sukkoth. Wakasafiri kutoka Sukkoth wakatua Ethami iliyoko katika mwisho wa

- 7 bara. Wakasafiri kutoka Ethami, wakarudi nyuma kwa Pi-hahiroth, mbele ya Baal-zefon: wakatua mbele ya Migdol.
- 8 Wakasafiri kutoka mbele ya Hahiroth, wakapita kati ya bahari hatta barani: wakaenda safari ya siku tatu barani mwa
- 9 Ethami, wakatua Mara. Wakasafiri kutoka Mara, wakafika Elim: na kwa Elim zilikuwako chemchemi thenashara za maji,
- 10 na mitende sabwini; wakatua huko. Wakasafiri kutoka Elim, wakatua karibu na
- 11 bahari ya Sham. Wakasafiri kutoka bahari ya Sham, wakatua katika bara ya
- 12 Sin. Wakasafiri kutoka bara ya Sin, wakatua Dofka. Wakasafiri katika Dofka,
- 14 wakatua Alush. Wakasafiri katika Alush, wakatua Refidim, pasipokuwako maji
- 15 watu wanywe. Wakasafiri kutoka Refidim, wakatua katika bara ya Sinai. Wakasafiri katika bara ya Sinai, wakatua
- 17 Kibroth-hattaava. Wakasafiri katika Kibroth-hattaava, wakatua Hazeroth. Wakasafiri kutoka Hazeroth, wakatua Rithma.
- 19 Wakasafiri kutoka Rithma, wakatua Rimmon-Perez. Wakasafiri kutoka
- 21 Rimmon-Perez, wakatua Libna. Wakasafiri kutoka Libna, wakatua Rissa. Wakasafiri kutoka Rissa, wakatua Kehelatha.
- 23 Wakasafiri kutoka Kehelatha, wakatua kwa mlima Sheper. Wakasafiri kutoka
- 25 mlima Sheper, wakatua Harada. Wakasafiri kutoka Harada, wakatua Makheloth.
- 26 Wakasafiri kutoka Makheloth, wakatua

27 Tahath. Wakasafiri kutoka Tahath, wa-
 28 katua Tera. Wakasafiri kutoka Tera, wa-
 29 katua Mithka. Wakasafiri kutoka Mithka,
 30 wakatua Hashmona. Wakasafiri kutoka
 31 Hashmona, wakatua Moseroth. Wakasa-
 firi kutoka Moseroth, wakatua Bene-yaa-
 32 kan. Wakasafiri kutoka Bene-yaakan, wa-
 33 katua Hor-hagidgad. Wakasafiri kutoka
 34 Hor-hagidgad, wakatua Yot-batha. Waka-
 35 safiri kutoka Yot-batha, wakatua Abrona.
 Wakasafiri kutoka Abrona, wakatua Ezion-
 36 geber. Wakasafiri kutoka Ezion-geber,
 wakatua katika bara ya Zin (ndio Kadesh).
 37 Wakasafiri kutoka Kadesh, wakatua kwa
 mlima Hor, mwishoni pa inchi ya Edom.
 38 Akapanda Harun mkohani mlima Hor
 kwa amri ya Bwana, akafa huko, mwaka
 wa arobaini baada ya kutoka kwa waana
 wa Israeli katika inchi ya Misri, mwezi wa
 39 tano, ya kwanza ya mwezi. Naye Harun
 mwenyi miaka mia na asharini na tatu,
 40 alipokufa kwa mlima Hor. Akasikia
 Mkanaani, mfalme wa Arad, aliyekaa Ku-
 sini pa inchi ya Kanaani, habari za kuja
 41 kwa waana wa Israeli. Wakasafiri kuto-
 42 ka mlima Hor, wakatua Zalmona. Wakasa-
 43 firi kutoka Zalmona, wakatua Punon. Wa-
 kasafiri kutoka Punon, wakatua Oboth.
 44 Wakasafiri kutoka Oboth, wakatua Iye-
 45 abarim, mpakani mwa Moab. Wakasafiri
 46 kutoka Iyim, wakatua Dibon-Gad. Wa-
 kasafiri kutoka Dibon-Gad, wakatua

- 47 Almon-diblathaim. Wakasafiri kutoka
 Almon-diblathaim, wakatua katika milima
 48 ya Abarim, mbele ya Nebo. Wakasafiri
 kutoka milima ya Abarim, wakatua katika
 inchi sawa ya Moab karibu na Yardeni
 49 kwa Yeriko. Wakatua kwa Yardeni, to-
 ka Bet-yeshimoth hatta kwa Abel-shittim
 katika inchi sawa ya Moab.
- 50 Bwana akamwambia Musa katika inchi
 sawa ya Moab karibu na Yardeni kwa
 51 Yeriko, akisema, Sema na waana wa Isra-
 eli, ukawaambie, Mtakapovuka Yardeni
 52 kwa inchi ya Kanaan, ndipo mtakapowa-
 fukuza wakaao inchi wote mbele yenu,
 na kuziharibu nakishi zao zote, na kuziha-
 ribu sanamu zao zote, na kuzivunjavunja
 53 za penyi juu zao : nanyi mtaitiisha inchi,
 mtakaa humo : kwani ninyi nimewapa
 54 inchi kuitiisha. Nanyi mtaimiliki inchi
 kwa kura kwa jamaa zenu ; wakizidi uta-
 wazidishia milki, wakipunguka utawapu-
 nguzia milki : killa itakakomwangukia
 mtu kura, ndipo kwake ; kwa makabila ya
 55 baba zenu, mtaimiliki. Nanyi kama ha-
 mtawafukuza wakaao inchi mbele yenu :
 ndipo wale, mtakaowasaza wao, watakuwa
 kama machomo machoni mwenu, na miiba
 mbavuni mwenu, nao watawasumbua ninyi
 56 inchini mkaamo. Hatta itakuwa nilivyo-
 thani kuwafanyia wao, ndivyo nitakavyo-
 wafanyia ninyi.

SURA 34.

BWANA akamwambia Musa, akisema,
 (2) Uwaamuru waana wa Israeli,
 ukawaambie, Mkija kwa inchi ya Kanaan,
 (hii inchi itakayowaangukia kuwa milki,
 3 inchi ya Kanaan kwa mipaka yake,) pembe
 yenu ya kusini itakuwa toka bara ya Zin
 kupita upande wa Edom, na mpaka wenu
 wa kusini utakuwa toka mwisho wa Bahari
 4 ya Chumvi kwa mashariki, na mpaka wenu
 utageuka kusini pa kupandia Akrabbim,
 na kupita njia ya Zin : na matokeo yake
 yatakuwa kusini pa Kadesh-Barnea ; nao
 utatoka kwa Hazaraddar, na kupita kwa
 5 Azmon ; nao mpaka utazunguka toka
 Azmon hatta kwa kijito cha Misri, na ma-
 6 tokeo yake yatakuwa baharini. Na kwa
 mpaka wa magharibi mtakuwa nayo ba-
 hari kubwa mpaka : huu mpaka wenu
 7 wa magharibi. Na huu mpaka wenu
 wa kaskazini, toka bahari kubwa mtashi-
 8 ka mlima Hor : toka mlima Hor mtashika
 pa kuingia Hamath ; na matokeo ya mpa-
 9 ka yatakuwa kwa Zedad : na mpaka uta-
 toka kwa Zifron, na matokeo yake yata-
 kuwa kwa Hazar-enan : huu mpaka we-
 10 nu wa kaskazini. Nanyi mtashika toka
 Hazar-enan hatta Shefam mpaka wenu wa
 11 mashariki : na mpaka utashuka toka She-
 fam hatta Ribla, upande wa mashariki wa
 Ain : na mpaka utashuka, utafika upande
 wa bahari ya Kinnereth kwa mashariki :

- 12 na mpaka utashuka hatta Yardeni, na matokeo yake yatakuwa kwa Bahari ya Chumvi: hii itakuwa inchi yenu kwa mipaka
- 13 yake pande zote. Musa akawaamuru waana wa Israeli, akisema, Hii inchi mtakayomiliki kwa kura, Bwana aliyoiamuru wapewe wale makabila tissia, nayo nussu ya
- 14 kabila: kwani kabila la waana wa Reuben kwa nyumba za baba zao, na kabila la waana wa Gad kwa nyumba za baba zao, wamepokea, nayo nussu ya kabila la Manasse
- 15 wamepokea, milki yao: makabila mawili nayo nussu ya kabila wamepokea milki yao ng'ambo ya Yardeni karibu na Yeriko kwa mashariki, litokeako jua.
- 16 Bwana akamwambia Musa, akisema,
- 17 Haya majina ya watu watakaowamilikishia ninyi inchi: Eleazar mkohani, na Isa mwana wa Nun. Na mkuu mmoja mmoja wa
- 18 killa kabila mtatwaa waimilikishe inchi.
- 19 Na haya majina ya watu: wa kabila la Yuda,
- 20 Kaleb mwana wa Yefunne. Na wa kabila la waana wa Simeon, Shemuel mwana wa Ammihud. Wa kabila la Benyamin,
- 22 Elidad mwana wa Kislon. Na wa kabila la waana wa Dan mkuu, Bukki
- 23 mwana wa Yogli. Wa waana wa Yusuf: wa kabila la waana wa Manasse mkuu,
- 24 Hanniel mwana wa Efod: na wa kabila la waana wa Efraim mkuu, Kemuel mwana wa Shiftan. Na wa kabila la waana
- 25 wa Zabulon mkuu, Elizafan mwana wa

- 26 Parnak. Na wa kabila la waana wa Issakar mkuu, Paltiel mwana wa Azzan.
 27 Na wa kabila la waana wa Asher mkuu,
 28 Ahihud mwana wa Shelomi. Na wa kabila
 29 la waana wa Naftali mkuu, Pedahel mwana wa Ammihud. Hawa aliowaamuru Bwana wawamilikishie waana wa Israeli inchi ya Kanaan.

SURA 35.

BWANA akamwambia Musa katika inchi sawa ya Moab karibu na Yardeni kwa
 2 Yeriko, akisema, Uwaamuru waana wa Israeli, wawape Walawi katika milki ya mali zao miji ya kukaa; na malisho ya miji ya kuizunguka mtawapa Walawi.
 3 Nayo miji itakuwa kwao ya kukaa; na malisho yao yatakuwa kwa nyama zao, na kwa mali zao, na kwa vyao vyote vilivyo
 4 hayi. Nayo malisho ya miji mtakayowapa Walawi toka boma la mji pande zote mi-
 5 kono elfu kwa nje. Nanyi mtapima nje ya mji kwa mashariki mikono elfeen, na kwa kusini mikono elfeen, na kwa magharibi mikono elfeen, na kwa kaskazini mikono elfeen, nao mji katikati. Ndiyo yatakayo-
 6 kuwa kwao malisho ya miji. Nayo miji mtakayowapa Walawi miji sita ya kukimbilia, mtakayomwekea mwuaji aikimbi-
 lie: na zayidi ya hii mtawapa miji aroba-
 7 ini na miwili. Miji yote mtakayowapa

- Walawi miji arobaini na minane, ile
 8 na malisho yao. Nayo miji mtakayotoa katika mali ya Waana wa Israeli, katika mingi mtatwaa mingi; na katika haba mtatwaa haba: killa mtu katika milki yake aimilikiye atawapa Walawi katika miji yake.
- 9 Bwana akanwambia Musa akisema,
 10 Uwaambie waana wa Israeli, ukisema nao, Mtakapovuka Yardeni kwa inchi ya
 11 Kanaan, bassi mtajiwekea miji kuwa miji ya kukimbilia kwenu; apate mwuaji amwuaye mtu kwa ajali kukimbilia huko.
 12 Nayo miji itakuwa kwenu makimbilio katika mkombozi damu: asife mwuaji kabla hajasimama mbele ya kusanyiko ahukumiwe. Nayo miji mtakayotoa itakuwa
 14 kwenu miji sita ya kukimbilia. Mtatoa miji mitatu ng'ambo ya Yardeni, na miji mitatu mtatoa katika inchi ya Kanaan;
 15 itakuwa miji ya kukimbilia. Kwa waana wa Israeli, na kwa mgeni, na kwake akaaye kati mwao, itakuwa miji hii sita kwa makimbilio: killa amwuaye mtu kwa ajali
 16 akimbilie huko. Lakini kama amempiga nacho cha chuma, naye amekufa, yeye
 17 mwuaji: mwuaji kuuawa atauawa. Na kama amempiga kwa jiwe la mkononi, awezavyo mtu kufa nao, naye amekufa, yeye mwuaji: mwuaji kuuawa atauawa.
 18 Akimpiga nacho cha mti mkononi, awezavyo mtu kufa nao, naye amekufa, yeye

- 19 mwuaji; mwuaji kuuawa atauawa. Mkombozi damu mwenyewe atamwua mwuaji:
- 20 akimkuta yeye atamwua. Na kama amemsukuma kwa machukio, ao kumtupia, akivizia, hatta akafa; ao mwenyi wadui amempiga kwa mkono, hatta akafa: aliyempiga kuuawa atauawa; yeye mwuaji; mkombozi damu atamwua mwuaji, atakapomkuta.
- 22 Lakini kama amemsukuma ghafula asiye na wadui, ao amemtupia kitu asipovizia,
- 23 ao kwa jiwe lo lote, awezavyo mtu kufa nalo, asipomwona, akimtupia hatta akafa, naye si adui wake, wala hakumtakia mabaya: ndipo kusanyiko wataamua kati yake mpigaji na mkombozi damu kwa hukumu
- 25 hizi: nalo kusanyiko watamtoa mwuaji mkononi mwake mkombozi damu, nao kusanyiko watamrudisha kwa mji wake wa kukimbilia, alikokimbia: naye atakaa humo, hatta kufa kwa mkohani mkuu, aliyetiwa mafuta matakatifu. Lakini kama mwuaji kutokea atatoka mipakani mwa
- 27 mji wake wa kukimbilia akimbiliako, naye mkombozi damu atamkuta nje ya mpaka wa mji wake wa kukimbilia, naye mkombozi damu akimwua mwuaji, haitakuwa
- 28 damu juu yake: kwa sababu imempasa kuka katika mji wake wa kukimbilia hatta kufa kwa mkohani mkuu: lakini baada ya kufa kwa mkohani mkuu mwuaji atarudi
- 29 kwa inchi ya milki yake. Bassi haya yatakuwa kwa sheria ya hukumu kwenu ka-

- tika vizazi vyenu makaoni mwenu mwote.
- 30 Killa amwuaye mtu, mwuaji atauawa kwa kanwa la mashahidi : lakini shahidi mmoja
- 31 hatamshuhudia mtu kwa kufa. Wala hamtakubali dia kwa maisha ya mwuaji, aliye-
- 32 stahili kufa : lakini kuuawa atauawa. Wala hamtakubali dia kwake aliyeukimbilia mji wake wa kukimbilia, arudi kukaa kati-
- 33 ka inchi, hatta kufa kwa mkohani. Ndivyo hamtainajisi inchi, mliyomo : kwani damu ndiyo inajisishayo inchi : wala haupatikani uselehisho wa inchi kwa damu iliyomwagika humo, illa kwa damu yake aliyomwaga.
- 34 Wala hutaitia uchafu inchi mkaayo niyi, nikaaye nami kati yake : kwani mimi Bwana nakaa kati ya waana wa Israeli.

SURA 36.

- N**AO walio juu ya baba za jamaa ya waana wa Gilead, mwana wa Makir, mwana wa Manasse, wa jamaa za waana wa Yusuf, wakakaribia wakasema mbele ya Musa, na mbele ya wakuu walio juu ya
- 2 baba za waana wa Israeli : wakasema, Bwana amemwamuru bwanangu kuwamilikishia waana wa Israeli inchi kwa kura : na bwanangu aneamriwa na Bwana kuwamilikishia milki ya Zelofehad, ndugu yetu,
- 3 binti zake. Nao wakiolewa na waana wo wote wa makabila ya waana wa Israeli, ndipo milki yao itatwaliwa katika milki ya

baba zetu, nayo itatiwa kwa milki ya kabila, litakalokuwa lao: ndivyo itakavyo-
 4 twaliwa katika kura ya milki yetu. Na itakapokuwa Yubile ya waana wa Israeli, ndipo milki yao itatiwa kwa milki ya kabila, litakalokuwa lao: ndivyo itakavyotwaliwa milki yao katika milki ya kabila la baba zetu.

5 Musa akawaamuru waana wa Israeli kwa neno la Bwana, akisema, Wasemavyo ka-

6 bila la waana wa Yusuf ndivyo. Hili neno aliamurulo Bwana kwa binti za Zelofehad, akisema, Waolewe nao waonao vema; illa katika jamaa ya kabila la babao wataolewa.

7 Wala haitabadilika milki ya waana wa Israeli kabila kwa kabila: kwani waana wa Israeli wataambatana killa mmoja na

8 milki ya kabila la baba yake. Na killa binti mwenyi milki katika kabila lo lote la waana wa Israeli atakuwa mkewe mmoja wa jamaa ya kabila la baba wake, wapate waana wa Israeli kuimiliki killa mtu milki

9 ya baba zake. Wala milki haitabadilika katika kabila moja kwa kabila jingine; kwani makabila ya waana wa Israeli wataa-

10 mbatana killa mmoja na milki yake. Hatta kama Bwana alivyomwamuru Musa, ndivyo

11 walivyofanya binti za Zelofehad: wakaolewa Mahla, Tirza, na Hogla, na Milka, na Noa, binti za Zelofehad na waana wa ndu-

12 gu za baba wao. Katika jamaa za waana wa Manasse mwana wa Yusuf wakaolewa,

ikakaa milki yao katika kabila la jamaa ya baba yao.

- 13 Hizi amri na sheria, Bwana alizowaamuru waana wa Israeli kwa mkono wa Musa katika inchi sawa ya Moab karibu na Yardeni kwa Yeriko.

MWISHO.